

LUGHA NA MITAZAMO YA WAZUNGUMZAJI WA *KĪNDIA NA KĪGĪCHŪGŪ*

KUHUSU UTAMBULISHO WAO WA KIJAMII

PERIS MWIHAKI NDUNG’U

**Tasnifu itakayowasilishwa katika Halmashauri ya Masomo ya Shahada za Juu kwa
Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili
Chuo Kikuu cha Egerton**

CHUO KIKUU CHA EGERTON

MACHI, 2023

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo

Tasnifu hii ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa na yeyote katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi: 

Tarehe: 20/02/2023

Peris Mwihi Ndung'u

AM12/14102/15

Idhini

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.



Sahihi:

Tarehe: 22-02-23

Dkt. R. M. Gacheiya

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu,
Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi: 

Tarehe: 22-02-23

Prof. C. Kitetu

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu,
Chuo Kikuu cha Egerton.

HATILINZI

© 2023, Ndung'u Peris Mwihaki.

Haki zote zimehifadhiwa na hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia yoyote ile pasi idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa mume wangu mpendwa Dkt. Benson Waiganjo Kanyingi kwa ushauri wake na kunipa moyo wakati huu wote nikifanya kazi hii. Pia kwa watoto wetu wpendwa Elvis Kanyingi, Lucius Ndung'u na Amirah Mugure kwa uvumilivu na kunipa motisha na nguvu ya kuhitimisha tasnifu hii.

SHUKRANI

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, fikra na nguvu ya kuandika na kuikamilisha tasnifu hii. Pili, ninatoa shukrani za pekee kwa wasimamizi wangu katika utafiti huu Dkt. Raphael Gacheiya na Prof. Catherine Kitetu kwa kukubali kuchukua jukumu la kusimamia kazi hii. Ninawashukuru kwa uvumilivu wao tokea hatua ya kuandaa pendekezo la utafiti hadi kukamilika kwa tasnifu. Nawashukuru kwa mafanikio na juhudi yao ya kusoma, kukosoa na kunishauri kwa umakini hadi kuhitimisha. Hata ingawa walikuwa na majukumu mengine, hawakusita kusoma kazi yangu na kunielekeza kwa subira. Ninawaomba dua kwa Mwenyezi Mungu awazidishie katika maisha yao ili waweze kuendelea kuwafaidi wengine katika masomo yao. Pia namshukuru msimamizi wangu wa hapo awali, Prof. Furaha Chai kwa mchango wake ulionifaa katika pendekezo la utafiti. Namuomba kheri katika Chuo Kikuu cha Pwani.

Tatu, ningependa kushukuru uongozi wa chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa fursa ya kuzamia katika masomo yangu. Ninawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Fasihi, Lugha na Isimu kwa mchango, wosia na mawaidha yao wakiwemo mwenyekiti wa idara Dkt. Walunywa, mwenyekiti wa awali katika idara Dkt. Kweya, pamoja na wahadhiri Prof. Bartoo, Dkt.Taib, Bw. Muindi, Bw. Kahiro, Bw. Kwambai na wengineo. Mungu awazidishie ili waendeleo kuwafaa wengine kielimu na kitaaluma. Nne, ninatoa shukurani za dhati kwa wanafunzi wenzangu, Melvin Ouma, Mildred Abonyo, Geoffrey Kibet na Victor Gatimu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kitaaluma kwa kipindi chote cha masomo. Nawaomba fanaka kiakademia na katika maisha yao.

Tano, ninatoa shukrani za dhati kwa mama yangu Bi. Margaret Wambui kwa malezi na mapenzi yake, maombi na kuwa na imani kwangu. Shukrani kwa baba na mama mkwe, Bw. na Bi. Kanyingi kwa kunipa motisha kila wakati na kunihimiza kujitahidi nisife moyo. Naishukuru familia yangu, mume wangu, Dkt. Benson Waiganjo Kanyingi kwa upendo, uvumilivu na ufadhili wake. Shukrani kwa watoto wetu, Elvis Kanyingi, Lucius Ndung'u na Amirah Mugure kwa mapenzi na uvumilivu wao wakati wote wa masomo yangu. Vile vile, shukrani zangu ziendee familia ya mjomba, Bw. na Bi. Mbogo Robert kwa kufadhili masomo yangu ya shahada ya kwanza, Mungu awabariki na awalinde siku zote. Mwisho, nawashukuru Purity Muthoni na Bw. Kabiru waliokuwa watafiti wasaidizi wangu. Walikuwa wa msaada kwangu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Kwa wengine ambao kwa njia moja au nyingine walinisaidia katika kufanikisha kazi hii, nawashukuru nyote Mungu awabariki. **ASANTENI SANA.**

IKISIRI

Mawasiliano ni mchakato unaohusisha uhawilishaji wa ujumbe pamoja na uundaji na udumishaji wa utambulisho baina ya wazungumzaji. Katika maingiliano, binadamu hujaribu kuunda, kuendeleza na kudumisha utambulisho wake wa kijamii kupitia lugha. Utafiti huu ulinuia kuchunguza maingiliano na mahusiano baina ya wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ na wazungumzaji wengine wa Kikikuyu kimazungumzo. Utafiti ulitilia maanani jinsi wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanavyounda na kuendeleza utambulisho wao wa kijamii katika hali ya mtagusano wa kilahaja. Binadamu huashiria utambulisho wao kupitia lugha hasa kwa jinsi wanavyoteua matumizi ya misimbo mbalimbali. Malengo matatu mahususi yaliongoza utafiti huu; kubainisha mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao. Pili, kutathmini sababu za kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu. Tatu, kuchanganua michakato ya kiisimu ya kiukaribiano ambayo wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huhusisha katika uundaji wa utambulisho wa kijamii. Utafiti uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Utambulisho wa Kijamii na nadharia ya Ukaribiano wa Kimawasiliano. Utafiti huu ulikuwa wa kithamano na ulizingatia muundo wa kimaelezo. Mbinu za mahojiano, na uchunguzi shiriki katika miktadha isiyo rasmi zilitumika katika ukusanyaji wa data. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua mshiriki mmoja ambaye alisaidia katika uteuzi wa washiriki 48 kupitia sampuli tajwa. Uchanganuzi na uchambuzi wa data ulikuwa wa kimaelezo na ulihusisha uandaaji wa tunukuzi ambazo zilitafsiriwa kwa Kiswahili na baadaye kuwasilishwa kwa maelezo na majedwali. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa watafitiwa walikuwa na mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao wa kijamii. Asilimia sabini ya watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa vibainishi vya utamaduni, desturi, mila, historia na lugha sawa huwapa utambulisho wao kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu. Hata hivyo, asilimia ishirini na saba ya watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa ‘Gĩkĩrĩnyaga’ kama lugha yao huwapa utambulisho tofauti kama Wakĩrĩnyaga na hawaoni haja ya kubadili usemi. Watafitiwa waliendeleza maafikiano kwa madhumuni ya kufanikisha mawasiliano na kukubalika. Hata hivyo, walisistiza mwachano ili kudumisha lahaja zao ambazo walikuwa na mtazamo kuwa zinaweza kufifia. Utafiti huu umetoa maarifa kuhusu utambulisho wa kijamii na pia mchango katika isimujamii kuhusu jinsi matumizi ya lugha huendeleza utambulisho wa mtumiaji lugha.

ABSTRACT

Communication is a process that involves the exchange of information, construction and maintenance of identity among communicators. During an interaction, an individual tries to construct, develop and maintain their social identity through language. The main aim of the study was to investigate interactions between Kĩndia and Kĩgĩchũgũ dialect speakers with other Kikuyu speakers. Specifically in consideration of how they use language to negotiate and maintain their social identity in dialect contact situations. People enact who they are and where they belong through language, primarily through their linguistic choices. During communication, when speakers of mutually intelligible but regionally different dialects of the same language meet, the outcome is linguistic accommodation. In this respect, the study sought to; establish perceptions of Kĩndia and Kĩgĩchũgũ dialect speakers in terms of their social identity. Secondly, to evaluate why Kĩndia and Kĩgĩchũgũ dialect speakers identify themselves as Kikuyu. Thirdly was to analyse the linguistic accommodation strategies involved in constructing and negotiating social identity. The study was guided by the Social identity theory and Communication accommodation theory. The study was qualitative and adopted a descriptive research design. For data collection, interview schedules and participant observation were used to capture the daily interactions of Kĩndia and Kĩgĩchũgũ dialect speakers with other Kikuyu speakers in the informal context. Purposive sampling was used, then snowball sampling in selecting 48 participants. Data analysis was descriptive in nature and involved the preparation of transcripts and translations to Kiswahili. Then the data was presented qualitatively. Findings of the study revealed that the participants perceptions of their social identity varied, positively and negatively. Seventy per cent of the participants expressed that the same culture, traditions, history and language form crucial markers in their social identity as Kikuyu. However, twenty-seven per cent were of the view that their dialects, Kĩndia and Kĩgĩchũgũ, give them a distinctive identity as Wakĩrĩnyaga. The participants accommodated their interlocutor for effective communication and a sense of belongingness. However, due to the belief that their dialects would 'die,' the participants diverged by maintaining to speak their dialects. The study offers valuable insight and knowledge into social identity and belonging from Kĩndia and Kĩgĩchũgũ dialects speakers providing a better understanding of language use and social identity in sociolinguistics.

YALIYOMO

| | |
|--|------|
| UNGAMO NA IDHINI | ii |
| HATILINZI | iii |
| TABARUKU | iv |
| SHUKRANI | v |
| IKISIRI | vi |
| ABSTRACT | vii |
| ORODHA YA MAJEDWALI | xi |
| ORODHA YA RAMANI | xii |
| ORODHA YA VIFUPISHO | xiii |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 Usuli wa Mada..... | 1 |
| 1.1.1 Utambulisho wa Kijamii..... | 2 |
| 1.1.2 Kikikuyu na Lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ..... | 4 |
| 1.2 Suala la Utafiti..... | 6 |
| 1.3 Madhumuni ya Utafiti..... | 7 |
| 1.4 Maswali ya Utafiti..... | 7 |
| 1.7 Ufafanuzi wa Istillahi..... | 9 |
| SURA YA PILI | 10 |
| MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA | 10 |
| 2.1 Utangulizi..... | 10 |
| 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Dhana ya Utambulisho..... | 10 |
| 2.2.1 Tafiti kuhusu Lugha na Utambulisho wa Kijamii..... | 10 |
| 2.2.2 Tafiti kuhusu Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ..... | 13 |
| 2.2.3 Tafiti kuhusu michakato ya kiisimu..... | 17 |
| 2.3 Misingi ya Nadharia..... | 18 |
| 2.3.1 Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii..... | 18 |
| 2.3.2 Nadharia ya Ukaribiano wa Kimawasiliano..... | 21 |
| SURA YA TATU | 23 |
| MBINU ZA UTAFITI | 23 |

| | |
|---|-----------|
| 3.1 Utangulizi..... | 23 |
| 3.2 Mkabala wa Utafiti | 23 |
| 3.3 Eneo la Utafiti | 23 |
| 3.5 Uteuzi wa Sampuli..... | 24 |
| 3.6 Ukusanyaji wa Data | 25 |
| 3.6.1 Uchunguzi Shiriki | 25 |
| 3.6.2 Mahojiano | 25 |
| 3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data | 26 |
| SURA YA NNE | 27 |
| UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA | 27 |
| 4.1 Utangulizi..... | 27 |
| 4.2 Mitazamo ya Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ | 27 |
| 4.2.1 Mitazamo chanya na hasi ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii..... | 27 |
| 4.2.2 Watafitiwa waliokubali na kutokubali kujiainisha na kutambulishwa na jamiilugha ya Wakikuyu..... | 28 |
| 4.2.3 Mitazamo chanya na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii..... | 30 |
| 4.2.4 Mitazamo hasi na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wa kijamii | 34 |
| 4.3 Matumizi ya Lugha..... | 45 |
| 4.3.1 Matumizi ya Lugha ya Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ..... | 45 |
| 4.3.2 Michakato ya Kiisimu ya Kiukaribiano..... | 49 |
| 4.3.2 Mitazamo ya Watafitiwa kuhusu Ubadilishaji Lugha | 55 |
| SURA YA TANO | 60 |
| MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | 60 |
| 5.1 Utangulizi..... | 60 |
| 5.2 Muhtasari wa Matokeo | 60 |
| 5.3 Hitimisho..... | 63 |
| 5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti | 64 |
| MAREJELEO | 65 |

| | |
|--|----|
| VIAMBATISHO | 71 |
| Kiambatisho A: Mwongozo wa Mahojiano na Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ | 71 |
| Kiambatisho B: Mwongozo wa Mahojiano na Viongozi wa Mtaa | 72 |
| Kiambatisho C: Makala ya Utafiti Yaliyochapishwa..... | 73 |
| Kiambatisho D: Kibali cha Kufanya Utafiti Kutoka NACOSTI..... | 74 |
| Kiambatisho E: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI..... | 75 |
| Kiambatisho F: Barua ya Idhini Kutoka Wizara ya Elimu | 76 |
| Kiambatisho G: Ramani ya Eneo la Utafiti la Mwea..... | 77 |
| Kiambatisho H: Ramani ya Lahaja za Kikikuyu..... | 78 |
| Kiambatisho I: Tunukuzi Kutoka Mahojiano ya Watafitiwa..... | 79 |
| Kiambatisho J: Tunukuzi Kutoka Mahojiano ya Rununu na Dr. Julius Gathogo. | 85 |
| Kiambatisho K: Mahojiano na Prof. Mwaniki Kabeca..... | 87 |
| Kiambatisho L: Mazungumzo kati ya Watafitiwa | 89 |

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|---|----|
| Jedwali 1:Uteuzi wa washiriki katika mahojiano | 24 |
| Jedwali 2: Asilimia ya watafitiwa waliokuwa na mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao wa kijamii na jamii ya Wakikuyu | 28 |
| Jedwali 3: Asilimia (%) ya Watafitiwa Wanaokubali na Wasiokubali Kujitambulisha na Jamii ya Wakikuyu..... | 29 |
| Jedwali 4: Konsonanti za Lugha ya Kikikuyu | 46 |
| Jedwali 5: Asilimia ya watafitiwa walio na mitazamo chanya na hasi kuhusu kubadilisha lugha kama njia ya kuafikana | 55 |

ORODHA YA RAMANI

| | |
|--|----|
| Kiambatisho G: Ramani ya Eneo la Utafiti | 77 |
| Kiambatisho H: Ramani ya lahaja za Kikikuyu..... | 78 |

ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|--------|---|
| k.v | kama vile |
| KILAFO | Kenya Indigenous Languages Forum |
| n.k | na kadhalika |
| TF | Tafsiri Yangu |
| Uk. | Ukurasa |
| UNHCR | United Nations High Commissioner for Refugees |

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Lugha ni kipengele muhimu ambacho huunganisha binadamu kimawasiliano katika jamii (Trudgill, 1992). Lugha ina majukumu muhimu ya kuashiria utambulisho wa kundi, mshikamano wa kikundi, utofauti na vilevile kama njia mojawapo ya kuelezea na kuhifadhi utamaduni wa jamii fulani. Mukhwana (2017) anakubaliana na hili anaposema kuwa majukumu ya lugha kijamii ni mawili; kama njia ya mawasiliano na chombo cha kujitambulisha na kikundi fulani cha kijamii. Kila wakati binadamu anatumia lugha kuwasiliana, utambulisho wake wa kikundi cha kijamii husika hudhihirika. Ngugi wa Thiong’o (1986) anasema kuwa lugha hubeba utamaduni nao utamaduni hubeba amali zote zinazofanya watumizi wa lugha wajitambue na kupata mahali halisi ulimwenguni. Lugha kama njia ya kuashiria utambulisho wa mtumiaji lugha inaendelezwa na mawazo ya wataalamu mbalimbali wa kiisimu. Thornborrow (2004), anasema kuwa njia mojawapo ya msingi katika uundaji na udumishaji wa utambulisho na jinsi ya kuunda mitazamo ya wengine kuwahusu ni kwa kupitia jinsi wazungumzaji wanavyotumia lugha.

Fowler (1985, anavyonukuliwa katika King’ei na Kobia, 2007) anasema “lugha sio tu njia ya kujielezea bali pia ni chombo kinachoashiria tabaka na hadhi ya mzungumzaji katika jamii” (Uk. 322). Edwards (2013), anasema kuwa lugha huhusishwa na mamlaka, utambulisho na uwezo wa wanajamii. Anaendelea kusema, “jamii yenye nguvu hupenyeza amali zake za kisiasa, kitamaduni na kijamii” (Uk. 32). Jamii nyonge kwa upande mwingine hulazimika kukana na kuacha mifumo ya maisha yao na kufuata mifumo ya jamii yenye nguvu. Wakinukuliwa na Mbugua (2016), Adams na Mburugu (1994), wanadai kwamba kuna wakati wazungumzaji hujinasibisha na kabila fulani na wakati mwingine kukana utambulisho huo kutokana na sababu mbalimbali. Adams na Mburugu (1994) wanatoa mfano wa Wameru na makundi mengine madogo katika eneo la Mlima Kenya ambao hujinasibisha na jamii ya Wakikuyu ilhali wakati mwingine hukana utambulisho huo. Makundi ya watu walio wachache hubaguliwa kwa sababu hawana

mamlaka katika jamii (United Nations High Commissioner for Refugees, UNHCR, 2017). Kutokana na misingi hii, makundi haya ya walio wachache hujaribu kupigania kutambuliwa na kupewa hadhi katika jamii hiyo kwa kujinasibisha nayo na kusesitiza utambulisho wao wa kijamii.

Ingawa kila lugha huendeleza utofauti wa aina yake katika jamii, kila lugha huwa na hadhi sawa (Wolfram & Schilling, 2006). Hata hivyo, ukweli ni kwamba watu wana mitazamo hasi au chanya kuhusu lugha au lahaja ambapo huzifungamanisha na hadhi ya juu au chini. Mitazamo hii kama matokeo ya fikra huathiri vitendo vya mtumiaji lugha kwa sababu kuna imani kuwa kwa kutumia lugha ambayo ina hadhi, mzungumzaji hupata hadhi ya juu. Mitazamo hii ndiyo hudunisha matumizi ya lugha ya jamiilugha inayohusika. Wazungumzaji huhamasishwa kubadili mtindo wao wa uneni kama njia ya kueleza makusudio yao kwa wengine. Kiwango ambacho binadamu hubadili mitindo ya kiuneni kufanana au kutofautiana ni mfumo wa kukubalika au kutokubalika katika jamiilugha fulani (Bhat, 2017). Ubadilishaji wa uneni ili mzungumzaji kukubalika na kudumisha utambulisho wake kijamii hutokea kwa minajili ya kuafiki matarajio au matamano ya wanaozungumza nao (Soliz & Giles, 2014). Giles na wenzake (1991) wanaendelea kudai kwamba, uamilifu wa dhana ya kubadili uneni ili kufanana au kutofautiana ni kuashiria na kufanikisha umoja au mshikamano wa wazungumzaji. Kila wakati wanajamii wanapotangamana kimazungumzo kuna nia ya kukubalika ambayo ndiyo huongoza na kushinikiza watumiaji lugha kutumia lugha kwa njia tofauti. Ubadilishaji wa uneni ni njia mojawapo ya kuonyesha uhusiano kati ya watumiaji lugha. Kila mazingira huwa na sifa za kipekee ambazo wazungumzaji huzingatia ili kujitambulisha au kukubalika na anayezungumza ama kutofautiana naye (Galloiset na wenzake, 1995).

1.1.1 Utambulisho wa Kijamii

Utambulisho ni dhana ambayo hutokana na maarifa alionayo mwanajamii kuhusu kikundi cha kijamii anachohusiana nacho na kujiona kama mmoja wa kikundi au jamii hiyo pamoja na hisia ambazo zimefungamanishwa na uwanachama wa kundi husika (Tajfel, 1981, 1982). Yaani watu hupata utambulisho wao kutokana na kategoria za kijamii ambazo wanajaiinisha nazo kama wanajamii (Hoggs & Abrams, 1988). Utambulisho wa kijamii huamuliwa wakati watu wanatambua nafasi yao katika jamii. Utambulisho wa kijamii umefungamanishwa na utamaduni

ambao huashiriwa kupitia lugha (Kramersch, 1998, 2013). Jinsi kikundi fulani kinatumia lugha hutegemea haja ama mahitaji ya kikundi husika, kama vile, kuhifadhi na kudumisha utambulisho kama wanajamii wa kikundi fulani cha kijamii (Trudgill, 2000; Thornborrow, 2004). Mahusiano ya kijamii, mielekeo na imani husaidia kuunda utambulisho wa kijamii na huongoza matendo ya wazungumzaji kimawasiliano (Mukhwana, 2008).

Wardhaugh (1986) anaeleza kuwa, kila mtu ana utambulisho wake unaojengeka kutokana na jinsi anavyohusiana na kushirikiana na watu wengine katika jamii. Utambulisho wa kibinafsi huundwa kupitia matumizi ya majina na zoezi linalohusika katika kupeana majina ambalo hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine (Thornborrow, keshatajwa). Pili ni utambulisho wa kijamii, ambao kulingana na Msanjila (2011), ni ule upekee wa jamii ambao unabainishwa kwa misingi ya kitamaduni ambayo iko tofauti na misingi ya tamaduni ya jamii nyingine. Kwa upande mwingine, Thornborrow, anadai kuwa utambulisho wa kijamii umefungamana na mitazamo ya watu wengine wala sio jinsi mtu anavyojitathmini. Anaendelea kusema kuwa mtu hujitambulisha au kujinasibisha na kikundi cha kijamii kwa uwezo wake kwa kuzingatia kanuni zinazoongoza matumizi ya lugha ya kundi husika. Utofauti wa kiisimu kati ya wazungumzaji huwa unasababisha wao kuwa na haja ya kuashiria umoja na mshikamano na ndiposa hubadili matamshi yao ili kufanana au kutofautiana na wanaozungumza nao. Katika hali hii, Thornborrow anadai kuwa wazungumzaji huwa wanajaribu kuunda utambulisho wao ili wakubalike kama wamoja katika jamii husika.

Wardhaugh (1986) anakubaliana na mawazo ya Thornborrow anaposema kwamba kuna utambulisho wa kundi la watu katika jamii ambalo hujipambanua na kujitofautisha na makundi mengine katika jamii moja kutokana na utofauti wa mitindo yao ya kuzungumza lugha husika. Makundi katika jamii huweza kuzuka kutokana na tofauti mbalimbali za kijamii kama vile, lugha, elimu, umri, jinsia, utamaduni n.k. Watu wanaofanana katika mojawapo ya vipengele hivyo hujirejelea kuwa wamoja na kuona fahari kutambulishwa kama kundi moja. Kwa mfano, kulingana na Karangi (2005) wazungumzaji wa kīgīchugu katika enzi za uhamaji walikuwa wanaendelea utambulisho tofauti tofauti. Kuna wakati walijitambulisha na Gīkūyū na Mūmbi, koo tisa za

Wakikuyu; *Anjiru, Ambũi, Agacikũ, Aceera, Angarĩ, Ethaga, Aithĩrandũ, Airimũ, Angũi na Aicakamũyũ*. Nyakati zingine walijiainisha na majina ya marika ya Irungu na Mwangi.

Kulingana na Kenyatta (1938) utambulisho wa kijamii katika jamii ya Wakikuyu ulitegemea mambo matatu makuu ambayo yaliashiria na kuendeleza umoja na mshikamano katika shughuli zote za kikabila. Ujamaa, ukoo na desturi za hirimu ndizo ziliunganisha na kuunda utambulisho wa Wakikuyu. Wakiuru (2013) anakubaliana na Kenyatta anapodai kwamba katika jamii ya Wakikuyu ‘*mbarĩ*’ ilikuwa na umuhimu kwa kuwa ilikuwa ikitumika kama kigezo cha kumpa mtu utambulisho. Kenyatta (1938) anadai kwamba mwanachama wa jamii ya Wakikuyu, alijua utambulisho wake hususan kwa kujitambulisha na ukoo maalum ambao ulitokana na ‘*rurĩrĩ rwa mbarĩ ya Mũmbi na Gĩkũyũ*’ yaani kabila la ukoo wa Mumbi na Gikuyu waliokuwa asili ya jamii ya Wakikuyu. Hivyo basi utambulisho wa jamii ya ‘*Agĩkũyũ*’ uliundwa kwa mwanajamii kuwekwa katika ukoo maalum, ambao ulihakikisha mshikamano wa kijamii na kuwapa nafasi ya kujitambulisha kama Wakikuyu. Kulingana na Kenyatta (keshatajwa) mtoto wa kwanza wa kiume alipewa jina la mzazi wa kiume upande wa baba na wa pili kama ni wa kiume alipewa jina la mzazi wa kiume upande wa mama. Vilevile, kama mtoto wa kwanza alikuwa ni wa kike alipewa jina la mzazi wa kike wa baba na wa pili jina la mzazi wa kike upande wa mama. Jamii ya *Agĩkũyũ* imekumbwa na mabadiliko kadhaa kijamii na kitamaduni lakini ruwaza ya kupeana majina ni kipengee mojawapo muhimu katika utambulisho wao ambacho kinaendeleza na kudumisha utambulisho wa Wakikuyu.

1.1.2 Kikikuyu na Lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ

Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni lahaja za lugha ya Kikikuyu pamoja na Ki- Embu, Ki-Mbeere, Ki-Mathira (huzugumzwa Mathira), na zile za Kaskazini (huzungumzwa maeneo ya Murang’ a na Nyeri) na Kusini (huzungumzwa maeneo ya Kiambu) (Rejelea Kiambatisho H, uk. 78). Hata hivyo, kutokana na sababu za kisisasa na kijiografia, lahaja za Ki-Embu na Ki-Mbeere zinatambuliwa kama lugha kamili wala sio lahaja za lugha ya Kikikuyu (Mutahi, 1977). Waita (2020), anasema, “Wakikuyu huzungumza lugha ya Kibantu iliyo na lahaja tano zinazojulikana kati ya watu wanaojitambulisha kama Wakikuyu. Lahaja hizi ni pamoja na Kabete-Metumi, Gaki, Mathira, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ” (Uk.28). Kulingana na Karangi (2005) lugha ya Kikikuyu ina

lahaja nne ambazo ni; Kaskazini (Nyeri), Kusini (Kiambu), Kati (Murang'a) na Mashariki (Kirinyaga). Anaendelea kusema kuwa wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ huzungumza lahaja ya Mashariki. Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hujumuishwa pamoja kama '*Gikĩrĩnyaga*' (Mwaniki, 2014), na huzungumzwa katika maeneo ya Kirinyaga. Kuna madai kwamba lahaja hizi zinaweza kufifia kutokana na upendeleo wa lahaja sanifu. Lahaja sanifu ya lugha ya Kikuyu imeainishwa tofauti na wataalamu mbalimbali; Mutahi (keshatajwa) anadai kuwa lahaja za kaskazini na kusini ndizo hutambuliwa kama sanifu kwa sababu ndizo hutumiwa katika maandishi hasa katika vitabu, ufasili wa Bibilia na utangazaji. Karangi (2005) anadai kuwa ile lahaja ya Kusini (Kiambu) ndiyo lahaja sanifu kwa sababu hutumika katika uchapishaji wa vitabu na katika vyombo vya habari. Madai ya kufifia kwa matumizi ya lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ yanashabihiana na maoni ya Githinji (2014), ambaye anadai kwamba kwa kufanya utafiti wa Kĩndia anajaribu kuzuia kuangamia kwa lahaja hii.

Kiisimu, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wameainishwa kama Wakikuyu kwa kuwa wao huzungumza lahaja zilizoainishwa kuwa ni za lugha ya Kikikuyu na hupatikana katika kaunti ya Kirinyaga. Kikikuyu ni lugha ya Kibantu iliyo katika kundi la lugha za Niger-Kongo (Greenberg, 1946; Guthrie, 1967). Asili ya Wabantu kulingana na Guthrie ni Afrika Magharibi, sehemu za nchi ya Cameroon na kuenea na kusambaa katika maeneo mbalimbali. Guthrie aliziainisha lugha za Kibantu kwa kuzingatia maeneo ya Kijiografia na lugha ya Kikuyu iliwekwa katika kategoria la E (E51) ambalo linahusisha Kamba, Embu, Meru, Tharaka, Chuka, Mwimbi. Nadharia nyingine inadai kuwa, Kikikuyu ni mojawapo ya lugha zinazounda kikundi cha '*Thagicu*' ambacho kinajumuisha makundi mengine kama vile Kimbeere, Kiembu, Kimwimbi, Kitharaka, Kigembe, Kitigania, Kimeru na Kikamba (Muriuki, 1974).

Romaine (2000) anasema kuwa katika jamii, mitazamo au maoni ya wazungumzaji kuhusu wao ni akina nani au utambulisho wao katika jamii, yanaweza kutofautiana na ushahidi wa kiisimu ambao huweka makundi ya wazungumzaji wanaozungumza lahaja mbalimbali kama wanajamii wa lugha moja. Anatoa mfano wa wazungumzaji wa Tourai na Aria katika Papua New Guinea ambao kwa misingi ya kiisimu hudhaniwa ni wazungumzaji wa lahaja za lugha moja lakini wao hujichukulia kama wazungumzaji wa lugha tofauti. Dhana hii inatokea kwa wazungumzaji wa

lahaja za Kikikuyu ambapo wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huchukuliwa kuwa wao si Wakikuyu hata ingawa kiisimu wameainishwa na kuwekwa katika kundi moja na Wakikuyu.

Ruri (2011, anavyonukuliwa katika Gituru, 2019) anadai kuwa wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huchukuliwa kuwa si Wakikuyu halisi kwa kuwa hazijaandikiwa othografia. Dhana hii anayoiangazia Gituru (2019) ilitoa mshawasha wa kutaka kuchunguza mitazamo walio nayo wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii. Utafiti uliweza kubainisha kwamba dhana ya sisi na wao ilidhihirika kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ambapo wanajiweka katika kikundi cha kijamii kama Wakĩrĩnyaga ambao wanadhaliwa na kutengwa na Wakikuyu wenzao ilhali wanakubali kuwa kitamaduni, kimila na kidehuri wao ni Wakikuyu.

1.2 Suala la Utafiti

Wazungumzaji wa lahaja tofauti za lugha moja wanapoingiliana kimazungumzo, kuna uwezekano wa kundi moja kubadili uneni ili kuafikiana au kujitambulisha na kikundi cha kijamii husika. Katika matumizi ya lugha, tofauti za kiisimu zinapofungamanishwa na lafudhi ya wazungumzaji husika, mitazamo chanya au hasi huendelezwa. Wanajamii wanapoendeleza mitazamo hasi kuhusu utofauti huu kwa wazungumzaji wa lahaja nyingine, wakati uo huo wanaukana utambulisho wao kama wanajamii na husababisha utengano miongoni mwa makundi ya kijamii. Hata ingawa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wameainishwa kama wanajamii wa jamii ya Wakikuyu, wakati mwingi wao hurejelewa na Wakikuyu wenzao kama ‘*Wakĩrĩnyaga*’ na Wakikuyu wenzao. Zaidi ya hayo, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huchukuliwa kuwa wenye hadhi ya chini miongoni mwa wazungumzaji wa Kikikuyu. Katika jamii ambapo lugha fulani zinahusishwa na hadhi ya juu kijamii au kiuchumi, wazungumzaji wenye hadhi ya chini wanaweza kuchagua kujitambulisha na lugha hizo ili kupata manufaa na mapendeleo yanayohusiana nazo. Hakuna utafiti wa kina unaohusisha wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanavyojiainisha na kujitambulisha katika jamii. Hivyo basi, utafiti huu ulijaribu kuziba pengo hilo kwa kushughulikia mitazamo wanayoendeleza kuhusu utambulisho wao wa kijamii na jinsi wanavyotumia lugha kuunda utambulisho wao wa kijamii.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu lilikuwa kuchunguza na kueleza jinsi wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hujitambulisha kwa kuzingatia jinsi wanavyotumia lugha. Malengo mahususi ni kama yafuatayo;

- i. Kubainisha mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii.
- ii. Kutathmini sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kujitambulisha na jamiilugha ya Wakikuyu.
- iii. Kuchanganua jinsi wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hutumia lugha na michakato ya kiisimu wanavyotumia kuunda au kuendeleza utambulisho wao.

1.4 Maswali ya Utafiti

- i. Je, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mitazamo ipi kuhusu utambulisho wao wa kijamii?
- ii. Je, ni kwa nini wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hujitambulisha na jamii ya Wakikuyu?
- iii. Je, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanatumia lugha kwa jinsi gani na huendeleza michakato gani ya kiisimu ili kusisitiza utambulisho wao?

1.5 Umuhimu wa Kuchagua Mada

Utafiti huu unachangia kuelewa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ na kutumika kama nguzo ya kurejelewa katika tafiti nyinginezo za kiisimu. Utambulisho ni dhana ambayo haijatafitiwa kikamilifu miongoni mwa wazungumzaji wa jamiilugha ya Wakikuyu. Kuna utata wa utambulisho hasa kwa wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ambao hubadili usemi wao ili kuunda utambulisho wao kama wanajamii wa Wakikuyu kwa sababu huwa wanachukuliwa ni wa hadhi ya chini. Hivyo basi, kuna haja ya kufanya utafiti huu ili kupata maarifa ya kina kuhusu jinsi watumizi wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hujitambulisha kuzingatia mtazamo wao. Kuendeleza uelewa wa mtafiti kuhusu utambulisho ni muhimu kwa sababu maarifa haya yanatoa mwanga wa haja ya kufanya utafiti zaidi hasa kuhusisha wanajamii wengine ambao wanatatizika kujitambulisha. Kutokana na uelewa huu, watafiti wengine watahamasishwa kufanya tafiti za utambulisho wa wazungumzaji wa lugha za Kiafrika. Matokeo ya utafiti huu ni mchango katika

taaluma ya Isimujamii kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha na utambulisho kwa kuzingatia jinsi matumizi ya lugha huendeleza utambulisho wa wazungumzaji katika jamii.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ni wa kiisimu hasa katika tawi la isimujamii. Watafitiwa walikuwa ni wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kwa sababu wao huchukuliwa kuwa ni wa hadhi ya chini miongoni mwa wanajamii wanaozungumza lugha ya Kikikuyu katika jamiilugha ya Wakikuyu. Mtafiti alichunguza mitazamo ya wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii na jinsi walivyotumia lugha kuunda na kuendeleza utambulisho huo. Mtafiti alichunguza jinsi washiriki waliendeleza mazungumzo kati ya wazungumzaji wa lahaja moja na wanapoingiliana na wazungumzaji wa lahaja tofauti katika miktadha ya kazini isiyo rasmi. Utafiti huu uliendelezwa kwa mazungumzo ili kutathimini matumizi yao ya lugha katika mazingira asilia na kubainisha michakato ya kiisimu wanayoendeleza. Washiriki waliotumiwa ni viongozi wa mitaa pamoja na wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Mtafiti si mahiri katika kuzungumza lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ jambo ambalo liliweza kumzuia kuwasiliana kwa urahisi na watafitiwa hivyo basi, mtafiti alitafuta mtafiti msaidizi ambaye ana uelewa zaidi kuhusu lahaja hizi na mazingira yaliyoteuliwa.

1.7 Ufafanuzi wa Istillahi

- Jamiilugha:** Kundi la watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamii moja ambayo iko tofauti na jamii nyingine.
- Lahaja:** Kitarafa cha lugha kinachobainika kijamii au kijiografia na kudhihirishwa na vipengele maalumu vya kisauti na kimuundo (Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha, 1990). Fasili hii inafaa katika utafiti huu kwa kuwa inazipa lahaja hizi hadhi sawa katika mawasiliano ya jamii husika.
- Lafudhi:** Upekee wa kutamka maneno ambao humtambulisha mtu binafsi na mwingine.
- Ukaribiano:** Hali ya kubadili uneni ili kupunguza au kuendeleza tofauti kati ya wazungumzaji.
- Utambulisho:** Hisia ambazo huelezea mtu binafsi ni nani na jinsi anavyohusiana na kundi jamii kwa misingi ya kitamaduni na lugha.
- Utambulisho wa kijamii:** Maarifa aliyo nayo mwanajamii kuwa yeye ni wa kikundi fulani katika jamii.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imetalii machapisho na tafiti mbalimbali ili kupata mawazo na maarifa ambayo yalitanguliwa kuhusu mada ya utafiti. Mtafiti ameshughulikia yalioandikwa kuhusu lugha ya Kikikuyu kwa jumla na yanayohusu lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, lugha na utambulisho na tafiti kuhusu michakato ya kiisimu. Pia, mtafiti amefafanua misingi ya nadharia ambayo itaongoza utafiti.

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Dhana ya Utambulisho

Dhana ya utambulisho ni pana kwa sababu inahusisha jumla ya vibainishi mbalimbali vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, makundi ya watu, jamii moja na taifa moja. Vibainishi hivi hubainisha kuwa kundi fulani ni tofauti na lingine, jamii moja ni tofauti na nyingine na kadhalika. Tabouret-Keller (1989, anavyonukuliwa katika Massamba et al., 2011) anadai kuwa utambulisho wa mtu umefungamana na mambo mengine k.v lugha, utamaduni, mavazi, vyakula, dini, historia ya jamii, siasa na uchumi. Edwards (2009) akirejelea fasili ya Groebner's (2004) anadai kwamba utambulisho ni mtazamo wa kibinafsi wa mtu, yeye ni nani na vibainishi viavyoashiria ushirika wa kikundi fulani katika jamii.

Utambulisho kulingana na Thornborrow (2004) ni dhana inayoundwa na kusisitizwa maishani kupitia kwa maingiliano ya watumizi lugha. Anaendelea kusema kuwa njia mojawapo ambayo utambulisho huundwa na kuendelezwa uwe wa kibinafsi au kijamii ni katika matumizi ya lugha yaani jinsi watumizi lugha huwasiliana na kuingiliana kimazungumzo. Ili kufaninikiwa kujitambulisha na kikundi cha kijamii, kuna maana kwamba watumizi lugha watabadili mitindo ya kiisimu ili kufanana na ya kundi hilo kwa jinsi wanavyotamka maneno na sauti husika (Thornborrow, 2004).

2.2.1 Tafiti kuhusu Lugha na Utambulisho wa Kijamii

Holmes (2013) anadai kuwa, jinsi lugha hutumika katika miktadha mbalimbali huashiria mahusiano ya kijamii na jinsi watu huunda na kuendeleza masuala ya utambulisho wa kijamii.

Lugha ni chombo muhimu katika jamii kwa kuwa husaidia wanajamii kuendeleza mahusiano na kudhihirisha mipaka ya utangamano wao. Ni kupitia lugha mtu huwa mwanajamii halisi kwani lugha humwezesha kujihusisha na kujitambua kama mmoja wa kikundi fulani cha kijamii ulimwenguni (Crystal, 2000). Mzungumzaji wa lugha hujitambulisha na jamii fulani kwa kuzungumza huku akizingatia kanuni na taratibu za jamii anayojinasibisha nayo. Kwa mfano, Mutahi (1977) anasema kuwa ili mzungumzaji wa lahaja ya Kĩndia au Kĩgĩchũgũ kujitambulisha kama Mkikuyu halisi atajaribu kuzungumza kwa kuzingatia matamshi ya sauti na kanuni za lugha sanifu ya Kikikuyu ili kuendeleza utambulisho wake wa jamii hiyo

Msanjila (2011) katika makala yake, anadai kuwa ili kubaini utambulisho wa mzungumzaji, vielelezo vya kijamii na kiisimu hutumiwa. Anaendelea kueleza kuwa vile vielelezo vya kiisimu ni pamoja na lahaja, lafudhi, kiimbo, matamshi ya sauti na hata miundo ya lugha na kadhalika. Vielelezo vya kijamii hufungamana na utamaduni wa jamii ya mzungumzaji. Utambuzi wa utambulisho wa mzungumzaji wa lugha au lahaja fulani hung'amuliwa kutokana na tofauti ambazo hujitokeza wakati wa mazungumzo. Tabouret-Keller na Le Page (1986, wanavyonukuliwa katika Msanjila, 2011) wanadai kuwa lugha na utambulisho haviwezi kutenganishwa kwani matamshi ya mzungumzaji ni matamshi ya utambulisho wake. Otuoma (2015) anaunga mkono maoni ya Msanjila anaposema kuwa, vibainishi vya uchumi, siasa, utamaduni, historia ya jamii, dini, mavazi na vyakula hutumiwa kuukamilisha utambulisho wa mtu. Ugunduzi huu unaashiria kuwa ni vigumu kubainisha utambulisho wa mzungumzaji kwa kutumia lugha pekee bila uchanganuzi wake kwa kuzingatia jamiilugha anayotoka ambako masuala ya utamaduni, mila na desturi ni sehemu muhimu na kiungo cha umoja wa jamiilugha hiyo. Jamiilugha inapojitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine katika masuala ya kimsingi kama vile utamaduni, mila, desturi na imani hudumisha na kutetea amali za jamii yao (Msanjila, 2011).

Theophil (2012) katika utafiti wake kuhusu lugha na utambulisho wa jamii ya Wahaya wanaoishi Dar es Salaam alilenga kubaini kama wanadumisha utambulisho wao kama Wahaya. Theophil alitathmini matumizi ya lugha ya Kihaya kwa kuzingatia muktadha wa kielimu, hata baada ya wao kuhama kutoka maeneo ya kijiografia ambayo Wahaya wanaishi. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa idadi kubwa ya wazungumzaji hawa wanadumisha utambulisho wao

kama jamii ya Wahaya kwa kuzungumza Kihaya hata ingawa wengine wao wanajitambulisha na jamii ya ujumla ya Watanzania kwa kuzungumza Kiswahili. Pia alizingatia kigezo cha umri na kubaini kuwa asilimia kubwa ya wazee ndiyo wanaoendeleza utambulisho wa jamii ya Wahaya ikilinganishwa na vijana hali ambayo huendeleza mwachano au utofauti kwa kuisitiza kuzungumza Kiswahili. Matokeo ya utafiti wa Theophil yalidhihirisha kuwa wazee ndiyo hudumisha utambulisho wao na jamii ya Wahaya wakilinganishwa na vijana. Matokeo haya yanawiana na matokeo ya utafiti huu kwani asilimia kubwa ya waliokubali kujitambulisha na jamiiligha ya Wakikuyu ilikuwa ni wazee ambao walisitiza kuwa wana historia, utamaduni, desturi sawa na ile ya Wakikuyu. Katika matumizi ya lugha pia, wazee walisitiza matumizi ya lahaja zao ilhali vijana walichanganya kwa kuingiza misamiati ya Kiswahili kwani hiyo ndiyo lugha wanayotumia kwa upana wakiwa shuleni.

Joho (2011) amefanya utafiti kuhusu matumizi ya majina katika utambulisho wa jamii ya Watanzania. Katika utafiti wake, Joho alilenga kubaini jinsi majina ya familia ambayo imekubalika kubeba dhana ya utaifa na utambulisho wa jamii ya Watanzania, majina ya matukio ya kihistoria na majina ya vivutio vya utalii kama vile mito na milima huitambulisha jamii pana ya Watanzania. Asilimia kubwa ya majina ambayo alichunguza, ilikubalika kuendeleza dhana ya utaifa na utambulisho wa jamii pana ya Watanzania bila kujali jina linatokana na jamii gani. Utafiti huu umeangazia kigezo kimoja cha majina ambacho hutumiwa kuendeleza utambulisho wa jamii fulani bila kuzingatia matumizi ya lugha katika miktadha tofauti, hivyo basi kuna pengo ambalo mtafiti anuia kuziba. Utafiti wa Joho ulichangia kuelewa jinsi wazungumzaji huendeleza utambulisho wa kijamii na mshikamano kama wanajamii kwa kuzingatia utamaduni katika matumizi yao ya majina. Kulingana na Joho, kuna yale majina ambayo yamekubalika kuashiria utambulisho wa jamii ya Watanzania, hali ambayo inapatikana katika kila jamii. Hata ingawa utafiti huu haukuangazia dhana ya matumizi ya majina katika utambulisho, ilidhihirika kuna yale majina ya kiukoo (Kenyatta, 1938), ambayo huwapa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ utambulisho wao kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu.

Githinji (2006) alichunguza jinsi wazungumzaji wa Sheng nchini wanavyojitambulisha katika makundi ya kijamii kwa uzingativu wa jinsi wanavyotofautiana kileksia na wenzao maeneo

ya Nairobi. Anagundua kuwa wazungumzaji kutoka mitaa ambayo ina mapato ya chini hubadili vipengele vya leksia ili kufanana na wale ambao wanatoka katika mitaa iliyofanikiwa kiuchumi. Anaendelea kueleza kuwa hata ingawa utofauti katika Sheng umeenea kwa mapana, kuna wazungumzaji ambao huwa wanasisitiza kutumia matamshi ya kimsingi ya Sheng ili kufanikisha mawasiliano. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa, kwa manufaa ya kujitambulisha, watafitiwa walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu msimbo huu wa Sheng ilhali wakati uo huo wao wanauona kama msimbo usio sanifu. Utafiti huu ulitathmini jinsi wazungumzaji hujitambulisha kama ‘sisi’ au ‘wao’ katika matumizi ya Sheng. Githinji alichunguza jinsi wazungumzaji wa Sheng huendeleza dhana ya utambulisho katika matumizi yao ya Sheng. Utafiti huu unawiana na matokeo ya utafiti huu kwa kuwa kuna asilimia ya watafitiwa walijiweka katika kundi ndani, ‘sisi’ kama Wakĩrĩnyaga na kujitenga na kundi nje, ‘wao’ yaani la Wakikuyu.

2.2.2 Tafiti kuhusu Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ

Kenyatta (1938) anasema kuwa Wakikuyu walijigawa katika makundi mawili makubwa, kundi la Kusini linalojulikana kwa jina Karura au Kabete, na kundi la katikati linalojulikana kama Murang’a, Mathira, Ndia na Embu. Ithanga ni eneo muhimu katika kuelewa historia ya Wakikuyu kwa kuwa makundi ya Waembu, Wambeere na Wakikuyu yalikutana na kutawanyika kuelekea maeneo mbalimbali kutoka eneo hili (Karangi, 2005; Kenyatta, 1938). Muriuki anakubaliana na madai haya anaposema kuwa makundi ya Waembu, Wambeere, Wandia, Wagichugu na Wakikuyu yalikutana na kutawanyika kutoka eneo la Ithanga. Anaendelea kusema kuwa, “Kutoka eneo la Ithanga waasisi wa jamii ya ‘Agĩkũyũ’ walisafiri katika makundi madogo madogo kuelekea Magharibi, huku wakiwaacha jamaa zao wengine ambao leo wanaunda wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ” (Uk.60). Zaidi ya hayo, anaendelea kusema kuwa baada ya kuwasili kutoka Ithanga, Wakikuyu walisambaa na kufanya makao yao katika maeneo ya Metumi, Gaki na Kabete na ndiposa anagawa Kikuyu katika lahaja tatu kuu ambazo ni Gaki, Metumi na Kabete ilhali wazungumzaji wa Ndia na Gichugu anawatambulisha kama binamu za Wakikuyu. Hata hivyo, Mutahi anaendelea kusema kuwa utamaduni kati ya wazungumzaji wa lahaja hizi za, Gaki, Metumi, Kabete, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni sawa. Maoni haya ya Mutahi, yalizua haja ya kuchunguza

mtazamo na msimamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii.

Middleton (1953, anavyonukuliwa katika Mbugua, 2016) anasema kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hurejelewa kama Wakikuyu hata ingawa kwa maoni yake wao hutofautiana kitamaduni. Maoni haya ya Middleton yanahitilifiana na matokeo ya utafiti huu kwani wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanakubali na kusisitiza kuwa utamaduni wao; ukoo, ruwaza ya kupeana majina, taratibu za ndoa ni sawa na ule wa jamiilugha ya Wakikuyu. Kwa mtazamo wake Muriuki, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni binamu wa karibu wa Wakikuyu pamoja na Wameru, Wambeere, Waembu, Wakamba na Wamaasai na kwamba kwa kuzingatia lugha, wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wamekopa kutoka Embu, Nyeri na Murang'a. Hata hivyo, Muriuki anatoa mtazamo kinzani kwamba, kwa kuzingatia utamaduni, wao ni Wakikuyu hasa kwa sababu walikuwa wakihusishwa katika mikutano ya kiukoo (Muriuki, 1974). Mtazamo huu wa Muriuki unasababisha utata wa utambulisho wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kwa kuwa, kulingana na Msanjila (2011) utambulisho ni dhana ambayo imejumuisha vibainishi vya utamaduni, mila na desturi, lugha, historia ya jamii, mavazi, chakula, imani na kadhalika. Maoni haya ya Msanjila, yanawiana na mitazamo waliosisitiza watafitiwa kuwa utambulisho wao kama wanajamii wa jamii ya Wakikuyu imejumuisha vibainishi hivi vya utamaduni, historia, mila na desturi sawa.

Uainishaji wa kikabila ambao ulifanywa mwaka wa 1948 na wakoloni, ulitambulisha wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kama wanajamii wa Waembu lakini katika mwaka wa 1962 kulitokea mabadiliko ambapo makundi haya mawili yaliainishwa kama Wakikuyu (Blacker, 2007). Uainishaji huu ulifanywa ili kuweka makundi mbalimbali katika makabila tofauti kirasmi nchini Kenya ambapo makundi mengine yalipewa hadhi ya kuwa kabila k.v Mbeere na Tharaka ambayo yalikuwa yameainishwa kama Waembu na Wameru mtawalia. *Kenya Indigenous Languages Forum* (KILAFO) ambacho ni kikundi kinachotetea udumishaji wa lugha za kikabila hasa 'Gĩkĩrĩnyaga', wanadai kwamba wazungumzaji wa 'Gĩkĩrĩnyaga' wana utamaduni na utambulisho tofauti na ule wa Wakikuyu. 'Gĩkĩrĩnyaga' kulingana na KILAFO ni lugha inayoundwa na lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ambazo huzungumzwa katika Kaunti ya Kirinyaga.

Kundi hili linaendeleza hisia kuwa kutokana na uainishaji wa ‘*Gikĩrĩnyaga*’ kama Kikikuyu, kuna uwezekano wa lugha hii na desturi zao za kitamaduni kuangaamia. Hivyo basi, wanapendekeza kwamba lugha hii itenganishwe na kabila za Wakikuyu, Waambu, Wambeere na Wameru ambao ni binamu zao na kupewa hadhi ya kabila la Wakĩrĩnyaga.

Mutahi (1977) katika utafiti wake wa mabadiliko ya sauti na uainishaji wa lahaja za Kusini mwa Mlima Kenya anaziainisha lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kama lahaja za Kikikuyu. Hata hivyo, anatambua kwamba lahaja hizi, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, zinapewa hadhi ya chini kutokana na sababu ya kuwa sio sanifu. Anaendelea kusema kuwa wazungumzaji wa lahaja zenye hadhi ya chini, k.m wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huwa wanashawishiwa na wale wenye idadi kubwa na hadhi ya juu kuzungumza ‘Kikikuyu’ yaani ile inayoaminika kuwa sanifu na kwamba hata wakati mwingine huwa wanapokea matusi kutokana na jinsi wanavyozungumza.

Mutahi (keshatajwa) anasema kwamba kuna shinikizo kwa wazungumzaji wa lahaja za chini kuzungumza lahaja iliyosanifiwa ili kuendeleza uhusiano wao na wale ambao wanazungumza lahaja sanifu. Gituru (2019, anavyonukuliwa katika Ruri, 2011) anadai kwamba wazungumzaji wa lugha za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huchukuliwa kuwa si Wakikuyu halisi kwa kuwa lugha hizi hazijaandikiwa othografia. Ruri (keshatajwa) anatilia mkazo maoni ya Mutahi (keshatajwa) kuwa wazungumzaji wa lugha ambazo hazijaandikiwa othografia hujikaza kuzungumza lugha iliyoandikiwa othografia ili kuthibitisha kwamba wao ni Wakikuyu halisi. Katika maelezo yake Ruri (keshatajwa), wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni baadhi ya walioathiriwa na hali anayoizungumzia Mutahi. Mutahi (keshatajwa), anadai kwamba wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanatatizika kujitambulisha kama wanajamii wa jamii ya Wakikuyu ‘halisi’ hasa kutokana na mitazamo na mielekeo hasi kwamba hawazungumzi Kikikuyu. Maoni haya ya utafiti wa Mutahi, yanaingiliana na matokeo ya utafiti huu kwani ilibainika kwamba watafitiwa waliendeleza mitazamo hasi kuhusu utambulisho wao kama Wakikuyu kwani wana hisia kuwa hawajakubalika na Wakikuyu wenzao kutokana na jinsi wanavyozungumza.

Kwa upande mwingine, Mutahi (keshatajwa) anatambua kwamba wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanakopa matumizi ya sauti zingine katika mazingira mengine na kuwa

hakuna ushahidi wowote ambao umetolewa kueleza hali hii mbali anakisia tu kwamba hali hii inaweza kuwa inasababishwa na kanuni ya Dahl's. Kanuni ya Dahl ni kanuni ya lugha iliyogunduliwa na Dahl, na kupewa jina katika mwaka wa (1903) na Meinhof, inahusu lugha za Kibantu ambapo ikiwa kuna konsonanti mbili ghuna moja hupoteza ughuna wake, au kama kuna mfuatano wa konsonanti mbili zisoghuna moja hufanywa ghuna (Makini, 2015). Utafiti huu wa Mutahi ulisaidia mtafiti katika uchambuzi wa data katika kuelewa tofauti zilizopo kati ya lahaja hizi kifonolojia na kimofolojia. Utafiti huu ulitofautiana na ule wa Mutahi kwa sababu ulizingatia tu kuchanganua mabadiliko ya usemi inayotokea kifonolojia.

Rosa (1981) katika utafiti wake, anadai kwamba Wabantu wa maeneo ya kati ni pamoja na Wakikuyu, Wandia, Wagĩchũgũ, Waambu na Wameru. Anaendelea kusema kuwa kwa mtazamo wa kiisimu na kijiografia, Wabantu wa kati wamegawika katika migao miwili mikuu; Wakikuyu na Wameru. Anaendelea kusema kwamba, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ katika wilaya ya Kirinyaga wana uhusiano wa karibu na Wakikuyu na hujitambulisha kama Wakikuyu hasa kunapotokea haja ya kutaka kujitambulisha. Hivyo basi, utafiti wa Rosa ulitoa mwanga ya kwamba kuna haja ama shinikizo kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kujitambulisha na kundi jamii la Wakikuyu.

Kamau (1996) amefanya utafiti wa mifanyiko ya kifonolojia kati ya lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Kwa kuzingatia vipengele vya irabu na konsonanti, anaweka wazi tofauti baina ya lahaja hizi kifonolojia. Pia anatathmini na kufafanua mageuzi ya kifonolojia. Githinji (2014) amefanya utafiti kuhusu lahaja ya Kĩndia kwa kuzingatia vipengele vya unazali, uwiano wa irabu na toni. Githinji (2014) anadai kwamba kwa mipaka ya maeneo ambayo wazungumzaji wa Kĩndia wanaishi, lahaja hii hupitia mabadiliko kutokana na athari za lahaja jirani kama vile Kĩgĩchũgũ na Kimathira. Anaendelea kusema kuwa lahaja hii huwa inatofautiana na lahaja sanifu ya Kikuyu (ambayo anadai ni ya Kaskazini na Kusini) kwa toni, muundo wa sauti na wakati mwingine leksia. Kwa upande mwingine, Wachera (2008) amechanganua toni kama kipengele cha kipekee katika leksia ya Kĩgĩchũgũ kama lahaja ya lugha ya Kikikuyu. Wachera (2008, anavyonukuliwa na Githinji, 2014) anasema kuwa toni huwa inadhihirika tofauti katika lugha ya Kikikuyu hasa kwa kuzingatia mahali na ruwaza zake. Utafiti huu ulishughulikia mabadiliko ya kilahaja iliyotokea

wakati wazungumzaji Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanapojaribu kufanana au kutofautiana na Wakikuyu ili kuunda utambulisho. Hivyo basi, tafiti hizi zilisaidia katika kuelewa na kuchambua fonolojia ya lahaja ya Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hasa katika kubaini mabadiliko yaliyotokea katika matumizi ya lugha baina ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ.

2.2.3 Tafiti kuhusu michakato ya kiisimu

Michakato ya kiisimu ambayo inlizingatiwa katika utafiti huu ni ile ya kiukaribiano inayodhihirika wakati wazungumzaji wanapobadilisha usemi wao ili kujitambulisha na kundi fulani cha kijamii hasa kwa kupunguza tofauti kati yao. Ukaribiano ni ile tabia inayoendelezwa na binadamu katika mazungumzo kwa minajili ya kuafiki matarajio au matamano ya wanaozungumza nao (Soliz & Giles, 2014). Hii ni dhana ambayo hutokea katika maingiliano ya kila siku hasa kutokana na mielekeo ya binadamu kuhusu lugha au aina fulani ya lugha inayotumiwa wanapowasiliana. Giles na wenzake, (1991) wanasema michakato hii ya kiisimu huwa na uamilifu wa kuashiria na kufanikisha umoja au mshikamano wa wazungumzaji katika mazungumzo. Michakato hii hutokea kati ya watu wenye lugha tofauti au wazungumzaji wa aina au lahaja mbalimbali za lugha moja. Kutokana na hali za mtagusano wa kilahaja au aina za lugha moja, mabadiliko mengi ya kiisimu huwa inatokea ambapo vipengele maalum huwa vinahawilishwa kutoka aina moja ya lugha hadi nyingine (Trudgill, 1986). Hali hii, kulingana na Trudgill, inaweza kuelezwa kwa ufasaha kwa kuzingatia ufanano na utofauti wa kiisimu ambao hutokea katika maingiliano ya wazungumzaji wa lahaja tofauti za lugha moja. Mzungumzaji hubadili lugha au aina ya msimbo ili kuafiki mahitaji ya mpokezi wake kama njia mojawapo ya kuonyesha uhusiano uliopo kati ya wazungumzaji hasa wanapojaribu kuunda utambulisho wao wa kikundi mahsusi cha kijamii.

Giles na Bourhis (1977) walitafiti matumizi ya lugha kati ya wazawa wa jamii ya Welsh huku wakizingatia utofauti ambao hutokea kilafudhi. Katika utafiti huu, wataalamu hawa waligundua kuwa wazungumzaji wa lugha hii walipohisi kuwa utambulisho wao wa kikabila unatishiwa waliendeleza matumizi ya lafudhi ya Ki-Welshi kwa mapana kwa kuwa walithamini mshikamano na umoja kama kundi. Katika utafiti huu, utambulisho wa jamii hiyo ya Welsh uliendelezwa kwa kusisitiza utofauti. Matokeo ya Giles na Bourhis yanashahibiana na ya utafiti

huu kwani wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ walisisitiza matumizi ya lahaja zao kwa hofu yazo kufifa. Utafiti wa Giles na Bourhis ulifaa katika uchambuzi wa data, hasa kuelewa dhana za kiukaribiano wanazoendeleza wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuunda utambulisho wao wa kijamii.

Kebeya (1997) alifanya uchunguzi wa ukaribiano wa kiisimu katika mtagusano kati ya lahaja mbili za Kiluhya; Lwitakho na Logooli huku akizingatia ufanano na utofauti ambao ni wa kifonolojia. Alibainisha kuwa wazungumzaji wa lahaja hizi huwa wanabadili sehemu za kifonolojia kwa namna tofauti hasa wanaendeleza ufanano na wanaozungumza nao. Mabadiliko hayo aiyajumuisha kama kaida za kifinolojia. Pia alieleza sababu kuu ambazo huwa zinasababisha wazungumzaji wa lahaja hizi kuendeleza ufanano na utofauti ambazo ni pamoja na; haja ya kufanikisha mawasiliano, haja ya ushirikiano na ukubalifu kwa wanaowasikiza, kujitambulisha na kundi ambalo linazungumza lahaja yao n.k. Kwa kuhitimisha, alipendekeza utafiti zaidi kufanywa kwa uzingativu wa vipengele vya kimofolojia, kileksia na kisintaksia katika lahaja zingine za Kiluhya. Utafiti huu unatoa mwanga wa jinsi maingiliano ya wazungumzaji wa lahaja za lugha moja huendeleza ukaribiano kwa uzingativu wa vidadiliki vya kijamii; umri, jinsia na kiwango cha elimu. Katika utafiti wetu, tunajaribu kuoanisha dhana ya utambulisho wa kijamii na matumizi ya lugha, hasa kuchunguza kama watafitiwa husika wanabadili matamshi yao ili kusisitiza utambulisho wao na jamiilugha ya Wakikuyu, hivyo kujaza pengo ambalo Kebeya hajazingatia.

2.3 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Utambulisho wa Kijamii iliyoasisiwa na Henri Tajfel na John Turner (1979), na nadharia ya Ukaribiano wa Kimawasiliano iliyoasisiwa na Giles (1973). Nadharia hizi zimeelezwa katika sehemu ifuatayo;

2.3.1 Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii

Nadharia hii iliasisiwa na kuendelezwa na Henri Tajfel akishirikiana na John Turner mwaka wa 1979. Kulingana na mawazo ya Tajfel na Turner, binadamu hujijengea silka ya kutaka kujitambulisha na kundi au jamii wanayohusiana nayo. Tajfel (1979) akirejelea suala la matumizi ya lugha anadai kwamba watu huwa wamegawika katika makundi mbalimbali na kila kundi

hutumia lugha kwa namna inayomtambulisha na kundi husika. Kwa kawaida watu wanaopenda kujitambulisha na jamii au kundi fulani huwa wanajichukulia wao wenyewe kuwa wapo sawa na ni wamoja. Binadamu hujijengea silka za kujitambulisha kwa kuhusisha michakato ya kiakili ambayo huhusisha kuwatathmini watu wengine kama “sisi” au “wao.” Michakato hii huhusisha mawazo matatu makuu yanayojumuisha mihimili ya nadharia hii ambayo ni;

- i. Ujiainishaji
- ii. Utambulishaji, na
- iii. Ulinganishaji wa kijamii.

Tajfel na Turner wanadai kuwa binadamu huainisha vitu ili aweze kuvielewa na kuvitambua, sawa na jinsi watu wanavyoainishwa. Ujiainishaji huhusisha kuainisha watu katika makundi au kategoria mbalimbali kama vile weupe, weusi, Mkenya, Mkikuyu, mwanafunzi, mwanamume na kadhalika. Watu huwekwa katika kategoria mbalimbali ili waweze kutambuliwa kwa urahisi. Watumizi lugha hujitambulisha kwa kuzingatia tabia na mienendo ya kundi au jamii husika.

Kipengele cha utambulishaji kijamii kulingana na wataalamu Tajfel na Turner, ni kwamba watumizi lugha hutwaa utambulisho wa kikundi mahususi ambacho wanajitambulisha nacho na kutenda kwa njia ambazo huendelezwa na watu katika kundi hilo. Kwa mfano, ikiwa mzungumzaji atajitambua kama Mkikuyu kuna uwezekano atatwaa utambulisho huo kwa kutenda akizingatia kaida ambazo zinaongoza kundi hilo na baadaye kudumisha utambulisho huo kama mwanachama wa kundi hilo. Baada ya binadamu kujiainisha kama sehemu ya kundi fulani na kujitambulisha na kikundi hicho, basi hujaribu kulinganisha kundi hilo na makundi mengine katika jamii. Ili kudumisha na kuendeleza utambulisho wa kikundi hicho cha kijamii, mtumizi lugha anaweza kubadili jinsi anavyotumia lugha. Mtumizi lugha anapotaka kudumisha hadhi yake, basi ni lazima ajilinganishe vyema na makundi hayo mengine, makundi ya nje.

Binadamu huainisha watumizi lugha katika makundi tofauti tofauti, ambao pia hujiweka katika makundi mbalimbali yaani utambulishaji wa kijamii. Baada ya kujiainisha na kujitambulisha na kikundi cha kijamii, watumizi lugha hutafuta namna zitakazowawezesha kukubalika katika kikundi hicho. Watumizi lugha husisitiza kuwa wanachama wa kundi ndani na

kuendeleza hisia chanya kuhusu kundi lao wanapojilinganisha na kundi nje ambalo wanaamini kuwa ni tofauti na lao. Katika utafiti huu watafitiwa walijiweka katika kundi ndani kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu na kukana utambulisho na makundi ya jamiilugha za Waembu na Wameru kutokana na lugha na utamaduni wao. Pia kuna asilimia ya watafitiwa ambao walipojilinganisha na Wakikuyu wengine walijihisi kama wanabaguliwa na kutengwa hivyo kujiweka katika kundi ndani kama Wakĩrĩnyaga. Kutokana na mawazo haya, Tajfel (1982) aliorodhesha vijenzi vitatu vya utambulisho ambavyo vinaendeleza misingi ya nadharia hii.

1. Kijenzi cha utambuzi. Mzungumzaji yeyote ana maarifa au anafahamu ya kwamba yeye ni mwanajamii wa kikundi fulani cha kijamii.
2. Kijenzi cha utathmini. Mzungumzaji anaweza kutathmini kwa njia chanya au hasi kundi fulani analojitambulisha nalo na ushirika wake katika kundi hilo.
3. Kijenzi cha kihisia. Mzungumzaji huendeleza hisia mahsusi za kukubalika au kutokubalika katika kikundi cha kijamii ambacho anajitambulisha nacho kupitia matendo yake.

Nadharia hii inafafanua umuhimu wa kuwa mwanajamii wa kikundi cha kijamii huwa na uelewa na ufahamu binafsi wa kinachomfanya kujinasibisha na kujitambua na kikundi hicho (Tajfel, 1982). Wanajamii wanapojitambulisha na jamii au kikundi fulani cha kijamii huwa na mtazamo kuwa kuna usawa kati yao na ni kitu kimoja. Nadharia hii ilitusaidia katika utafiti huu kwa sababu ilituwezesha kutambua vibainishi vinavyosababisha wazungumzaji kuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu utambulisho wao wa kijamii. Vibainishi hivi vya utamaduni, mila, desturi na lugha vinayowaunganisha kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu. Utambulisho wa aina hii ndio msingi wa jamiilugha kutetea na kudumisha amali za jamii yao. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuelewa mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ katika kujijengea silka ya kujitambulisha kupitia lugha wanayotumia katika miktadha mbalimbali. Vilevile, nadharia ya utambulisho ilisaidia kubainisha uelewa na ufahamu walio nao wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao. Hata hivyo, haikusaidia mtafiti katika kuchunguza michakato ambayo huendelezwa kujitambulisha hasa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanapobadili

mitindo ya uneni na ndiposa mtafiti alichagua nadharia ya pili; Nadharia ya Ukaribiano wa Kimawasiliano.

2.3.2 Nadharia ya Ukaribiano wa Kimawasiliano

Nadharia hii iliasisiwa katika miaka ya 1970 kama nadharia ya ukaribiano wa kiuneni (Giles, 1973; Giles et al., 1973), na kuendelezwa na Giles na Coupland (1991) kama nadharia ya ukaribiano wa kimawasiliano. Wataalamu hawa wana madai kwamba binadamu hujitahidi kuzungumza au kuiga lugha ya msikilizaji wake ili kukidhi haja ya mawasiliano. Mtumizi lugha huiga lugha ya mshiriki mwenzake kimazungumzo kwa kujua au kutojua, kufikiria au kutofikiria. Kulingana na Gallois et al. (2005) nadharia hii inapendekeza kuwa binadamu hubadili mitindo ya kiuneni kwa minajili ya kuunda na kusesitiza utambulisho wa kijamii. Nadharia hii hueleza mabadiliko yanayotokea katika matumizi ya lugha au uneni wa mazungumzo ya kila siku kwa kuzingatia mazingira halisi. Mabadiliko haya hutokea wakati wazungumzaji wanajaribu kusesitiza au kudumisha utambulisho wao na kikundi fulani cha kijamii. Nadharia hii ina mawazo yafuatayo;

- Kuna mfanano na utofauti wa kiuneni na kitabia katika kila mazungumzo;
- Lugha na tabia huwa ni viashiria vya hadhi ya kijamii na mshikamano wa kundi fulani;
- Mawasiliano huathiriwa na namna watu wanavyopokea na kutathmini kinachoendelea katika mazungumzo, yaani namna gani watu wanatafsiri na kuhukumu ujumbe uliobadilishwa katika mazungumzo; na
- Mawasiliano hubadilika kulingana na kaida na hali ya kimuktadha.

Nadharia hii hueleza dhana ya utambulisho kwa kuhusisha michakato miwili mikuu; ufanano na utofauti.

Giles na Coupland (1991) wanafasili ufanano kama mchakato ambao unahusisha watu kubadilisha mitindo yao ya kimawasiliano katika vipengele mbalimbali vya kiisimu ili kufanana na wanaozungumza nao. Mzungumzaji anapobadili jinsi anavyotumia lugha kwa kuiga matamshi ya mwingine, basi anajaribu kudumisha mshikamano na umoja wa kikundi hicho huku akijaribu kuendeleza utambulisho wa kijamii. Giles anafafanua kuwa sababu kuu ya kubadili mtindo wa matamshi ni kuonesha makubaliano na uhusiano walio nao wazungumzaji. Kwa upande mwingine,

wanafasili utofauti kama njia ambayo wazungumzaji husisitiza umbali wa kijamii au kuendeleza tofauti kwa kutumia vipengele vya kiisimu ambavyo vinawatambulisha kama kundi mahususi.

Nadharia hii ilikuwa muhimu katika kuchunguza michakato ambayo wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ waliendeleza ili kujitambulisha na kikundi husika. Nadharia hii ilisaidia kuonyesha mshikamano na uhusiano walio nao wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao kwa kufanana au kutofautiana kwa kuzingatia lugha na utamaduni wa jamii ya Wakikuyu

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mbinu ambazo zilitumika katika utafiti zinaelezwa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo; mkabala na muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, jinsi ya kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti ni mpangilio au utaratibu ambao huongoza ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Creswell (1998) anapendekeza utafiti wa kithamano kama mkabala mwafaka katika kuchunguza masuala tofauti ambayo hudhihirishwa na wanajamii katika mazingira halisi au asilia ya kijamii. Utafiti huu ulizingatia muundo wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Kothari (2004) tafiti za kimaelezo ni zile ambazo hutumika kupima viwango vya tabia fulani ya binadamu kwa kuifafanua ili kudhihirisha ni nini haswa huwasukuma watu kutenda au kusema namna wanavyotenda katika jamii.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanywa katika jimbo la Kirinyaga, eneo bunge la Mwea. Eneo bunge hili la Mwea limegawika katika kaunti ndogo za Mwea Mashariki na Mwea Magharibi. Mwea Mashariki imegawanywa katika kata tano na Mwea Magharibi ina kata mbili. Utafiti huu ulijikita katika eneo la Mwea kwa sababu kuna mchanganyiko wa wazungumzaji wa Kĩndia, Kĩgĩchũgũ na Kikikuyu kwa asilimia kubwa ikilinganishwa na maeneo mengine (Mutahi, keshatajwa). Mtafiti alichagua kinasibu kufanya utafiti katika vijiji vitatu vya Kiamanyeki, Maendeleo na Gathigiriri, katika kaunti ndogo ya Mwea Mashariki kwa kuzingatia uwepo wa wakazi wengi ambao ni wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Rejelea ramani ya eneo la utafiti katika Kiambatisho F Uk.77.

3.4 Sampuli Lengwa

Sampuli lengwa ni kundi la watu au vitu ambavyo vinaweza kuhusishwa katika uchunguzi kwa sharti la kuwa na sifa na vigezo linganifu (Orodho & Kombo, 2002). Utafiti huu ulilenga kuchunguza wazungumzaji wa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wa jinsia ya kiume na kike. Washiriki wa utafiti waliteuliwa kuanzia umri wa miaka ishirini hadi walio na zaidi ya miaka themanini ambao wanaishi maeneo ya Mwea Mashariki. Katika kigezo cha jinsia, mtafiti alizingatia idadi sawa ili kuleta uwiano sawa wa kijinsia katika uwakilishi na uelewa wa dhana ya utambulisho wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kijamii.

3.5 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuteua idadi ya watu kutoka ile sampuli lengwa ambayo itawakilisha idadi ya jumla katika utafiti (Orodho, 2009). Uteuzi wa kimaksudi ulitumika kuteua vijiji vitatu halafu sampuli tajwa ilitumika kuteua washiriki ambao wanazungumza lahaja ya Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Kiongozi mmoja wa mtaa aliteuliwa kimaksudi halafu alimsaidia mtafiti kuteua mshiriki mmoja ambaye aliwataja washiriki wengine ambao walisaidia katika utafiti. Washiriki 15 na kiongozi wa mtaa katika kila kijiji waliteuliwa kwa kuzingatia jinsia, umri na lahaja wanayozungumza. Kulingana na Milroy (1987) tafiti za kiisimu, huzalisha data yenye uradidi mwingi kwa kuwa kadri data ilivyo kubwa ndivyo kunatokea uwezekano wa uradidi. Hivyo basi idadi wakilishi ya watafitiwa 48 kutoka vijiji vitatu ilichaguliwa kutumika katika utafiti huu. Mtafiti aliongeza wasomi wawili walio na maarifa kuhusu watafitiwa ili kufafanua zaidi kuhusu suala la utafiti.

Jedwali 1: Uteuzi wa Washiriki katika Mahojiano

| Umri | Kijiji 1 | | Kijiji 2 | | Kijiji 3 | | Jumla |
|--------------|----------|------|----------|------|----------|------|-------|
| | Kiume | Kike | Kiume | Kike | Kiume | Kike | |
| 20-39 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 12 |
| 40-59 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 12 |
| 60-79 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 12 |
| 80 -90 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 12 |
| Jumla | 8 | 8 | 8 | 8 | 8 | 8 | 48 |

3.6 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data unahusisha vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti na mbinu za ukusanyaji wa data nyanjani. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu za uchunguzi shirikishi na mahojiano.

3.6.1 Uchunguzi Shiriki

Hii ni mbinu ambayo ukusanyaji wa data huendelezwa kwa kushiriki na kutazama matukio katika mazingira asilia. Mbinu hii huwa na manufaa ya kupata ufahamu wa kina kuhusiana na mada ya utafiti na kuelewa jamii au watafitiwa kwa njia mwafaka (Milroy & Gordon, 2003). Pia mtafiti hukusanya data ya hali ya juu kwani anaangazia matukio ya jamii kwa undani kwa kuzingatia mitazamo yao. Mbinu hii imepungukiwa kwa sababu huwa inachukua muda mwingi. Hata hivyo, kulingana na Milroy na Gordon (2003) watafiti wanaweza kufikia manufaa ya mbinu hii kwa kutumia muda kidogo, kwa kujenga muamana na watafitiwa. Milroy na Gordon (2003), wanasema kuwa kuendeleza muamana na watafitiwa ni njia moja ya kupunguza upendeleo wa watafitiwa wanapoendeleza mazungumzo yao katika mazingira asilia. Mtafiti alijenga muamana na watafitiwa na kushirikiana na watafitiwa katika shughuli za kil siku kwa muda wa mwezi mmoja. Mazungumzo yote yaliyoendelezwa katika mazingira mbalimbali ikiwemo sokoni, nyumbani na hotelini yalimsaidia mtafiti katika uchanganuzi wa jinsi watafitiwa walitumia lugha na michakato ya utofauti na ufanano iliyoendelezwa. Mtafiti aliendeleza mahojiano kwa madhumuni ya kupata ufafanuzi kuhusu haja na sababu za kuendeleza utambulisho wa kijamii.

3.6.2 Mahojiano

Mahojiano ni njia ya kuuliza maswali ana kwa ana kwa namna ya mazungumzo kati ya mtafiti na mtafitiwa (Kothari, 2008; Orodho, 2009). Mahojiano ni ya aina mbili; funge na huru. Mahojiano funge yalimsaidia mtafiti kupata data ya kimsingi kuhusu mtafitiwa. Mahojiano yalihusisha uundaji wa maswali yaliyoendeleza majibu katika mazungumzo na pia maswali yaliyotumiwa kuelewa mitazamo ya watafitiwa na jinsi wanavyozungumza. Mtafiti alipata ujumbe wa kimsingi kuhusu watafitiwa au wazungumzaji kupitia mahojiano na kurekodi katika shajara kwa minajili ya uchanganuzi wa data baadaye. Mtafiti aliongozwa na mwongozo wa mahojiano ambao umeorodheshwa katika Kiambatisho A na B.

3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Kutokana na hali ya kuwa data ilihusu lugha ya Kikikuyu, mtafiti alizingatia hatua zifuatazo kuichanganua. Kwanza mtafiti alisikiliza data iliyorekodiwa na kuandaa tunukuzi za mazungumzo ambazo wasailiwa waliendeleza katika mahojiano na katika uchunguzi shirikishi. Mtafiti alifanya tafsiri ya moja kwa moja mazungumzo yaliyonukuliwa kutoka lugha chanzi ya Kikikuyu hadi Kiswahili. Data ilipangwa kwa utaratibu ambao ulijibu maswali au madhumuni ya utafiti na kuchanganua yaliyomo. Uwasilishaji wa data ulifanywa kimaelezo ambao ni mkabala unaoeleza jinsi matukio katika mazungumzo yanavyotokea na kuwasilishwa katika majedwali ili kuonyesha utambuzi wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu, jinsi walivyojitathmini kuhusu utambulisho wao na vipengele vya kifonolojia ambavyo vilibadilishwa kimazungumzo.

3.8 Maadili ya Utafiti

Katika utafiti, maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote mtafiti hutangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu (Mukuthuria, 2009). Ili kuhakikisha kwamba uwajibikaji na uwelekevu wa utafiti huu ulitimizwa, mtafiti alitafuta idhini ya utafiti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Baadaye, mtafiti alijitambulisha kwa mkuu wa elimu katika jimbo la Kirinyaga na kupewa kibali cha kukusanya data katika eneo hilo. Halafu nyanjani mtafiti alijulisha chifu na viongozi wa vijiji katika eneo la utafiti kuhusu utafiti na madhumuni ya utafiti ili kupata kibali cha kutangamana na washiriki. Vilevile, washiriki walielezwa madhumuni ya utafiti ili mtafiti kupata kibali cha hiari yao ya kutaka kushiriki katika utafiti. Hakuna mtafitiwa aliyelazimishwa kushiriki katika ukusanyaji wa data.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao imejadiliwa. Katika utafiti, mtafiti alitaka kubainisha mitazamo na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii na jinsi mitazamo hii huathiri jinsi wanavyotumia lugha. Hivyo mtafiti amechanganua matumizi ya lugha na michakato ya kiismu ambyo walihusisha katika mazungumzo yao. Utambulisho ni hali ya jamiilugha fulani kujihisi na kung'amua kuwa iko sawa au tofauti na nyingine kwa misingi ya lugha, utamaduni, siasa, rangi, na kadhalika. Ili kuelewa utambulisho wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, kwanza mtafiti aliangazia ufahamu na uelewa wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu mifumo mbalimbali ya jamii wanayojitambulisha nayo.

4.2 Mitazamo ya Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ

Mitazamo kuhusu lugha au utambulisho wa wazungumzaji ni hisia walizo nazo watu kuhusu lugha yao au kuhusu lugha za watu wengine na ambayo hujengwa kiwakati kutokana na tajriba (Crystal, 1992). Iliidhihirika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao wa kijamii ambayo inaashiriwa katika jedwali 2 (katika ukurasa 28). Mtafiti alibainisha asilimia ya wazungumzaji waliokubali na kutokubali kujiainisha na kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu na matokeo yanaashiriwa katika jedwali 3 (katika Uk.29). Mitazamo na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ iliyoibuka kuhusu utambulisho wao wa kijamii inaelezwa katika sehemu hii.

4.2.1 Mitazamo chanya na hasi ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii

Utafiti huu ulibainisha kwamba watafitiwa walikuwa na mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao. Hisia chanya zilizojitokeza zilihusisha ukubalifu wa watafitiwa kunasibishwa na jamii ya Wakikuyu kwa kuwa wana lugha, utamaduni, desturi na mila sawa. Mitazamo hasi ilihusisha watafitiwa kubaguliwa, kudhalilishwa na kutengwa kutokana na lahaja

wanazozungumza, walizojumuisha kama *Gikĩrĩnyaga*. Matokeo kuhusu mitazamo chanya na hasi yalikuwa kama inavyoashiriwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali 2: Asilimia ya watafitiwa waliokuwa na mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao wa kijamii na jamii ya Wakikuyu

| Mitazamo | Idadi ya watafitiwa | Asilimia |
|----------|---------------------|----------|
| Chanya | 30 | 62.5 |
| Hasi | 18 | 37.5 |
| Jumla | 48 | 100 |

NB: Data kutoka nyanjani.

Kutokana na matokeo katika jedwali 2, ni dhahiri kuwa asilimia 62.5 ya watafitiwa waliendeleza mitazamo chanya kuhusu utambulisho wao wa kijamii. Hata hivyo, asilimia 37.5 ya watafitiwa walikuwa na mitazamo hasi kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu na kuendeleza mitazamo kuwa wangependu kutambulishwa kama *Wakĩrĩnyaga* kwa kuwa wana imani kuwa wana tamaduni na lugha tofauti na ile ya Wakikuyu.

4.2.2 Watafitiwa waliokubali na kutokubali kujianisha na kutambulishwa na jamiilugha ya Wakikuyu.

Utambulisho wa mzungumzaji hauhusishi tu mzungumzaji kuwa na sifa bainifu za utambulisho wa jamii anayojihusisha nayo bali pia awe tayari kukubali kwamba yeye ni sehemu ya jamiilugha hiyo na kwamba anakubali kudumisha lugha na utamaduni wa jamii hiyo (Msanjila, 2011). Ili kubainisha watafitiwa waliokubali/kutokubali kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu, mtafiti aliwauliza wanajitambulisha na jamiilugha gani na walitoa majibu ambayo yanaashiriwa katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 3:Asilimia ya Watafitiwa Wanaokubali na Wasiokubali Kujitambulisha na Jamii ya Wakikuyu

| Makundi watafitiwa na umri | ya kulingana | Idadi watafitiwa | ya | % ya wanaokubali | % ya wasiokubali |
|----------------------------|--------------|------------------|----|------------------|------------------|
| 20-40 | | 16 | | 56 | 44 |
| 41-60 | | 12 | | 67 | 33 |
| 61 -90 | | 20 | | 90 | 10 |

NB: Data kutoka nyanjani.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa asilimia 90 ya watafitiwa wazee, asilimia 67 ya watafitiwa wa umri wa kati na asilimia 56 ya watafitiwa vijana walikubali kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu. Asilimia kubwa ya waliokubali kuwa wao ni wanajamii wa Wakikuyu ni wazee, huku vijana wakiwa na asilimia ndogo. Hii ni kwa sababu wazee wanaelewa mengi kuhusu asili, historia, utamaduni, mila na desturi za jamii yao wakilinganishwa na vijana. Wazee huwa muhimu kurithisha na kuendeleza maswala yote ya jamii kwa vijana. Mikakati ambayo ilikuwa muhimu katika urithishaji huu haipo sasa kwani vijana wengi huenda shule katika maeneo tofauti ambapo hawapati nafasi ya kuelewa maswala ya utamaduni, historia ama desturi zao. Asilimia 90 ya watafitiwa wazee wanaokubali na kuendeleza utambulisho wa Wakikuyu wanadai kuwa utambulisho wa kijamii unazingatia vipengele vingi hasa vya kitamaduni ikiwemo lugha. Wazee walikubali kuwa lahaja wanazozungumza zina utofauti kwa kiasi na zile lahaja zingine za Kikikuyu lakini kuna uelewano kati ya Wakikuyu wote sababu lugha ni moja na watu wamoja.

Kulingana na matokeo yaliyo katika jedwali 3, asilimia 44 ya vijana hawakubali kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu ikilinganishwa na asilimia 10 ya wazee huku rika la kati likiwa na asilimia 33. Vijana wengi hawaoni haja ya kutambulishwa kama Wakikuyu bali wana mtazamo kwamba, ingekuwa mwafaka kama wanatambuliwa kama Wakirinyaga. Kwa mtazamo wao, hakuna manufaa au umuhimu wowote wa kuainishwa kama Wakikuyu, Waembu na kadhalika. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja aliashiria kuwa na mtazamo hasi aliposema, “mimi sijui ni kwa nini tunawekwa pamoja na hao ‘Akabete’ na kuitwa Wakikuyu. Ingekuwa vyema kama

tunatambulishwa kama ‘Wakĩrĩnyaga’ sababu tunazungumza lugha yetu, *Gikĩrĩnyaga*.” Kwa mujibu wa mtafitiwa huyu, *Gikĩrĩnyaga* ni lugha ambayo inajumuisha Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ambazo kwake anasema kuwa kiisimu hazina utofauti mkubwa. Mtafitiwa huyu alikuwa na mtazamo kuwa lugha ni kipengele muhimu katika utambulisho wao na kwa kuwa wanazungumza lugha tofauti na Wakikuyu, inapaswa watambuliwe kama Wakĩrĩnyaga.

4.2.3 Mitazamo chanya na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao wa kijamii

Kulingana na Tajfel (1979) mzungumzaji huwa anajiainisha na kikundi fulani cha kijamii ambacho huwa anatwaa utambulisho wake kwa kutenda huku akizingatia kaida za kundi husika. Kauli hii ilibainika kutokea katika utafiti kwa kuwa wengi wa watafitiwa walijitambulisha na jamii ya Wakikuyu huku wakisisitiza kuwa wanatenda kwa kuzingatia utamaduni, historia ya jamii ya Wakikuyu uliokubalika. Kwa mfano, mtafitiwa alisema, “*Nĩ ndĩ Mũgĩkũyũ nĩ tondũ rũciarwo rũakwa rumĩte gwĩ Gĩkũyũ na Mũmbi Kũhikania ni Ũgĩkũyũ, kũracia ona gũthĩnja igongonainĩ rĩa athuri ngwĩka o ta ũrĩa Ũgĩkũyũ wĩtikĩritie nĩkĩo ndĩreĩta Mũgĩkũyũ*”. (Mimi ni Mkikuyu kwa sababu mimi ni zao la Gikuyu na Mumbi Kuo, kutoa mahali, kuchinja katika sherehe za wazee kwa kufuata utaratibu unaokubalika katika jamii ya Wakikuyu Ndiyo maana najivunia kuitwa Mkikuyu) **(Rejelea Kiambatisho I, uk.79).**

Kutokana na dondoo hili, mtafitiwa anaendeleza mtazamo chanya kuhusu utambulisho wake kwa kujihusisha na jamii ya Wakikuyu kwa sababu ya historia na kuwa anazingatia kaida na taratibu za jamii husika. Mtafitiwa anaendeleza maoni kuwa utambulisho wake kama mwanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu umefungamana na utamaduni wa Wakikuyu. Mfumo au mpangilio wa kijamii unahusisha mambo mbalimbali k.v utamaduni, asili au historia, koo, ujinaishaji, malezi, elimu, ndoa, kifo na kadhalika. Utamaduni huipa jamii upekee na kuifanya kutambuliwa kwa njia maalum. Kauli inasisitizwa katika nadharia ya utambulisho wa kijamii, Tajfel (keshatajwa), anapofafanua kuwa utambulisho unazingatia vibainishi mbalimbali vya kisaikojamii vinavyofanya kundi fulani la jamii lijihisi kuwa liko na kundi lingine la jamii kwa kuendeleza maarifa ya jamii yake na mazoea ya pamoja ya kundi hilo.

Watafitiwa waliojitathmini na kujiainisha na jamii ya Wakikuyu walidai kuwa wanafuata mila na desturi sawa za Wakikuyu. Hili lilidhihirika katika matamshi ya mshiriki mmoja aliposema, “*ündũire wa Mũndia na Mũgĩkũyũ nĩ ùmwe*” (utamaduni wa ‘Mundia’ na Mkiikuyu ni sawa) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 81)**. Walijiainisha na kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu kwa sababu ya kuendeleza na kudumisha mfumo wa kiukoo unaokubalika katika jamii ya Wakikuyu. Kwa kujumlisha wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ, mtafitiwa mmoja alisema,

Dondoo 1: Tunukuzi kutoka mahojiano:

Agĩchũgũ ti Maembu, nĩ Agĩkũyũ tondũ mĩbĩrĩga yao yambĩrĩrĩe o ta ùrĩa mĩbĩrĩga ya Agĩkũyũ yambĩrĩrĩe, ùrĩa nĩ ya Anjiru, Agachikũ, Ambui, Angũi, Aitheradũ ùrĩa tũgaga nĩ ‘mĩbĩrĩga kenda muiyuru’ tondũ mũgĩkũyũ ndataraga indo ciake akarĩkia. Makĩria ma mĩbĩrĩga rĩ nonjuge mĩkarĩre na mĩtugo ya Agĩchũgũ, Andia, andũ ma Nyĩrĩ, Muranga na Kĩambu nĩ ùmwe tiga tu o rũthiomi. (Agĩchũgũ si Waembu bali ni Wakikuyu kwa sababu mfumo wao wa kiukoo ni sawa na ule wa Wakikuyu ikiwemo Anjiru, Agachiku, Ambui, Angui, Aitheradu ambayo ni tisa iliyokamilika, yaani kumi, sababu ni mwiko kwa Mkiikuyu kuhesabu mali yake kwa ukamilifu. Zaidi ya mfumo wa kikukoo mienendo na tabia za Agichugu, Andia, na Wakikuyu wengine waliotoka Nyeri, Muranga na Kiambu ni sawa isipokuwa tu jinsi tunavyotamka) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 81)**.

Historia na desturi zinazojulikana na wote katika jamii hujenga uhusiano wenye nguvu kati ya watu. Kuwa na udhibiti wa historia yako mwenyewe ni jambo muhimu; ujuzi wa historia huwapa watu utambulisho wao na huwafanya waungane zaidi na hutoa hisia ya "sisi", ndani ya kikundi na nje (Guse & Samuelsson, 2009). Watafitiwa wana mitazamo chanya kuhusu utambulisho wao kwani wanajivunia kutambulishwa kama Wakikuyu kutokana na mfumo wa kiukoo wa jamiilugha ya Wakikuyu. Watafitiwa walidai kuwa wanazingatia na kuendeleza koo tisa ambazo zinatokana na mabinti tisa wa Gĩkũyũ na Mũmbi. Koo hizi hutambuliwa kuwa “*Kenda mũiyurũ*” yaani tisa iliyokamilika sababu ilikuwa muhali kuhesabu vitu hadi kumi katika jamii ya Wakikuyu. Koo hizi ni kama zifuatavyo; Wanjikũ-Agacikũ, Wangari -Angari (Aithekahuno), Wambura -Ambura (Ethaga), Wamũyũ -Aichakamũyũ, Wairimũ -Airimũ (Agathigia), Wacera-Achera, Wambũi- Ambũi, Wangũi- Angũi (Athiegeni), Wanjirũ- Anjirũ na Wangeci -Angechi

(*Aitherandũ*). Katika utafiti watafitiwa walikuwa wakijinasibisha na koo kama ambazo kwao zinawapa utambulisho wao kama Wakikuyu k.v *Mũnjirũ, Mũceera, Mwethaga, Mũgacikũ, Mũmbũ* na zinginezo. Kwa mfano kulikuwa na kauli zifuatazo, “*nĩ ndĩ mũnjirũ na mũnjirũ njũt ni Mũgĩkũyũ*”, (mimi ni Munjiru na Munjiru ni Mkikuyu), mwingine alisema, “*ndĩ mũgĩkũyũ tondũ ndĩ wa mũbĩrĩga wa mũceera*” (mimi ni Mkikuyu sababu ukoo wangu ni Muceera). “*Rĩrĩa ndĩrauga ndĩ Mũgĩkũyũ nĩ tondũ wa mũbĩrĩga wakwa nĩ wa Angũi, ndikĩrĩ Mũngũi*”. (Wakati ninasema mimi ni Mkikuyu, ni kutokana na ukoo wangu ni wa Angũi, hivyo mimi ni Mũngũi) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 80)**.

Ujiainishaji na ujitambulishaji na jamii ya Wakikuyu pia ulisisitizwa na watafitiwa wa lahaja ya Kĩndia, kwa mfano kuna mtafitiwa aliyedai kuwa, “*Mũndia ni Mũgĩkũyũ nĩ tondũ wa nyũmba ĩrĩa ya mũbĩrĩga kenda mũiyũrũ kũmana na airĩtu a Gĩkũyũ na Mũmbi, no nĩ tondũ wa maĩ rĩ, mũario itũ ĩgĩchenjia*.” (Mundia ni Mkikuyu kwa sababu ya koo tisa kamilifu kutoka kwa mabinti wa Gĩkũyũ na Mũmbi lakini kutokana na maji matamshi ikabadilika) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 80)**. Mtafitiwa huyu alikuwa na mtazamo kwamba mfumo huu wa ukoo ndiyo unampa nafasi ya kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu. Kwa kulisitiza uhusiano wa karibu kati ya watu wa ukoo mmoja, umoja na mshikamano wa kijamii huendelezwa. Koo hizi zinaendeleza mshikamano wa wanajamii na kuwapa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ nafasi ya kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu. Kulingana na watafitiwa watu kutoka koo moja walikuwa wakishirikiana katika shughuli zote za jamii. Zaidi ya kuwepo kwa koo mbalimbali ambazo watafitiwa wanadai ziliwapa utambulisho na jamiilugha ya Wakikuyu, kulikuwa na mfumo wa rika. Hata ingawa mfumo huu hauzingatiwi katika jamii ya Wakikuyu kwa sasa, watafitiwa hasa wale wazee walisema kuwa baada ya kutahirishwa kila kijana aliwekwa katika rika fulani, kwa mfano rika la Maina, Irungu, Mwangi na kadhalika. Kulingana na watafitiwa mfumo huu uliendeleza mshikamano kati ya watu wa rika moja.

Katika utafiti ilibainika kwamba kuna ile hali ya kujitambulisha kwa kujigawa katika makundi ya “sisi” na “wao”. Kwanza watafitiwa ambao walizungumza Kĩndia walijitambulisha kama ‘*Wandia*’ kabla ya kujitambulisha kama Wakikuyu, hali ambayo ilitokea pia kwa watafitiwa wa Kĩgĩchũgũ. Hata hivyo asilimia tisini ya watafitiwa wazee walisema kwamba kwanza wao ni

Wakikuyu na kuendeleza kujitambulisha na lahaja wanayozungumza. Kwa mfano, “*niĩ ndĩ Mũgĩkũyũ Mugĩcũgũ*” (Mimi ni Mkikuyu Mugichugu). Anafafanua zaidi kwa kusema, “*ndĩrauga ndĩ Mugĩkũyũ mbere tondũ kũu nĩkĩo kĩhumo gĩakwa*” (Natangulia kusema mimi ni Mkikuyu kwa sababu hiyo ndiyo asili yangu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 80**). Wakikuyu wengine kutoka maeneo ya Murang’a, Nyeri na Kiambu walijumlishwa pamoja kama ‘Akabete’, ‘Wahaha’, ama ‘Wahihi’. Kwa mtazamo wao wanadai kwamba tofauti kati yao na ‘Wahaha’ inasababishwa na jinsi wanavyozungumza kilafudhi ingawa lugha ni moja. Hili lilisisitizwa katika kauli hii, “*ũtiganu wa Gĩgĩcũgũ na kĩrĩa gitagwo Gĩkũyũ nĩatĩ ũkiuga ‘haha’ niĩ ndĩrauga ‘aba’ but they can understand one another*” (tofauti baina ya Kĩgĩchũgũ na Kikikuyu ni kwamba unaposema ‘haha’ mimi ninasema ‘aba’, hapa, lakini wanaweza kuelewana) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 80**). Mtafitiwa anazungumza kwa Kiingereza ili kusesitiza kwamba hakuna utofauti wa mzungumzaji anayezungumza Kĩgĩchũgũ na Kikikuyu sababu ni wanajamii wa jamiilugha moja ya Wakikuyu.

Katika mahojiano na watafitiwa mbalimbali, dhana ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kunasibishwa na jamii zingine hasa Waembu na Wameru ilijitokeza kwa wingi na waliendeleza mitazamo hasi. Kwa wale watafitiwa waliodai kunasibishwa na Wameru na Waembu kwa wakati mmoja au mwingine walikuwa na mtazamo kwamba jambo hili linaudhi na kukera. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alieleza kuwa kuna wakati alitambulishwa kama Muembu na hakufurahishwa na jambo hilo hivyo alitaka kujua sababu mwenzake alimtambulisha kama Muembu, ambapo alielezwa kwamba ni kutokana na matamshi yake. Hata hivyo hakukubali kunasibishwa na jamii ya Waembu na akamweleza, “*niĩ ndirĩ Mũembu kana Mũmeru, ndĩ Mũgĩkũyũ wa Kĩrĩnyaga*” (Mimi sio Muembu wala Mmeru bali mimi ni Mkikuyu wa Kirinyaga) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 82**). Kauli hii inawiana na mawazo ya Tajfel (1982) anapodai kwamba, mzungumzaji yeyote huwa na maarifa kuwa yeye ni mwanajamii wa kundi fulani la kijamii na hukana utambulishaji na jamii nyingine. Hivyo basi, kijenzi cha utambuzi wa ushirika wa jamiilugha ya Wakikuyu kinabaika kwa kuwa watafitiwa wanakana utambulishaji na jamii za Waembu na Wameru na kusesitiza kwamba wao ni Wakikuyu.

4.2.4 Mitazamo hasi na sababu za wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wa kijamii

Katika utafiti ilibainika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mitazamo hasi kwamba wao hudhalilishwa, hutengwa, hukanwa na hudunishwa kama wanajamii wa jamii ya Wakikuyu kama anavyodai Mutahi (1983) anaposema kuwa katika jamii ya Wakikuyu, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huchukuliwa kuwa duni na wenye hadhi ya chini. Hali hii ya udunishaji wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ inatokana na mielekeo na mitazamo hasi ya Wakikuyu wenzao kutoka maeneo mengine ya Nyeri, Murang'a na Kiambu. Wazungumzaji wa lugha au lahaja duni au zenye hadhi ya chini wanapokubali na kusisitiza kuwa wanatengwa au kubaguliwa na wazungumzaji wa lugha au lahaja zilizo na hadhi, wanakuwa na hisia hasi kwa makundi hayo na hukana na kusisitiza utambulishaji wao kama kundi tofauti (Swim & Stangor, 1998). Maoni haya ya Swim na Stangor yanashinikizwa katika kauli za watafitiwa katika dondoo 2 na 3 zifuatazo;

Dondoo 2: Tunukuzi kutoka mahojiano:

Andũ ma Kĩrĩnyaga tutĩtikagĩrwo nĩ marĩa angĩ, no njũge tũtũ Kĩng'uruinĩ ona kana kĩng'ethũinĩ tũrĩ o bau" (watu wa Kĩrĩnyaga hatujakubalika na wale wengine, Wakikuyu, yaani hatutambuliwi kijamii) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 80).**

Dondoo 3: Tunukuzi kutoka mahojiano:

Akĩrĩnyaga tũhuana njagathi ya mbũũrĩ, tũtũ rũinĩ, tũtũ Embu, tũtũ Gĩkũyũinĩ. Īthũũ tũhuana ta maĩ me irũtũinĩ" tondũ tutirendwo. Kwaboteka uguo? Aca, kaba tumanwo na Agikuyu nĩguo tugĩe na recognition itũ ĩ mũndũ agĩe social dignity na pride yake ta Mũkĩrĩnyaga. (Akĩrĩnyaga huwa hatutambuliwi kama kundi la kijamii, sio Waembu wala Wakikuyu. Sisi tuko kama 'maji yanayoning'inia katika jani la nduma kwa kuwa tunakanwa. Hilo linawezekana? Hapana afadhali tujitenge na Wakikuyu tuwe na utambulisho wetu kama kundi ili mtu apate hesima na fahari kama Mũkĩrĩnyaga) **(Rejelea Kiambatisho J, uk. 86).**

Kauli za watafitiwa zinaashiria kuwa wamekubali kuwa wanatengwa na kubaguliwa na ndiposa wanasisitiza utambulishaji wao kama kikundi tofauti kama Wakĩrĩnyaga. Mtazamo huu wa kubaguliwa na kutengwa na wanajamii wenzao unawiana na maoni ya Mutahi (keshatajwa)

kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hurejelewa na Wakikuyu wenzao kama kama ‘mekamo’ yaani kiwele likiwa na maana kwamba hawawezi kutambulishwa na jamiilugha ya Wakikuyu wala jamiilugha ya Waambu. Hili linazua hisia hasi miongoni mwa watafitiwa na ndiposa wanaukana utambulisho wao kama wanajamii wa jamiilugha ya Wakikuyu na kutaka kujitega no na kutambulishwa kama Wakĩrĩnyaga.

Suala la wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kukanwa kama Wakikuyu ama Waambu linawiana na maoni ya Ngure na Karuru (2015), wanapozungumzia kuhusu utambulisho wa wazungumzaji wa Ariaal ambao wakati mwingine hunasibishwa na jamiilugha ya Warendille na wakati mwingine hukanwa kuwa si Warendille na kunasibishwa na jamiilugha ya Samburu. Ndiposa wanajirejelea kama ‘*maĩ marĩa me irũtũinĩ.*’ Kwa mtazamo wao lugha pekee si kibainishi tosha kwa watumizi lugha kujitambulisha na kikundi fulani cha kijamii, lazima kuzingatia maswala mengine ya kitamaduni, mila, desturi.

Dondoo 4: Tunukuzi kutoka mahojiano:

Ithuĩ ta Andia twatukana na Agĩchũgũ twĩ commonality atĩ tũtirĩ twetĩkĩrwo nĩ arĩa angĩ, maugaga atĩ nĩ kwĩringĩrĩria tũrerĩngĩrĩria”. (Sisi kama wazungumzaji wa Kĩndia na wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ kwa pamoja hatujawahi kukubalika na wale Wakikuyu wengine wao husema kwamba tunajilazimisha kutambuliwa kama Wakikuyu) (**Rejelea Kiambatisho J, uk. 86**).

Dondoo 5: Tunukuzi kutoka mahojiano:

I can say that they usually force themselves to be regarded or recognized as Kikuyu. Reke njuge ati, andu aya me thina tondu matiacceptwo ni Mugikuyu, matiacceptwo ni Muembu, mahuana ta maĩ marĩa tugaga me irũtũinĩ. (Naweza kusema kuwa ni kama huwa wanajilazimisha kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu. Watu hawa wana shida sana kwa kuwa wanakanwa na Wakikuyu, wanakanwa na Waambu, wanakaaa kama maji yaliyo katika jani la nduma ambayo huyumbayumba pande zote bila msimamo) (**Rejelea Kiambatisho K, uk. 87**).

Pia, watafitiwa waliokuwa na mitazamo hasi kuhusu utambulisho wao kama Wakikuyu walieleza kuwa huwa wanadhaliwa, wanatengwa na kubaguliwa na Wakikuyu katika hali

mbalimbali kwa sababu wanadhaniwa kuwa wao sio Wakikuyu wala ‘*andũ ma nyũmba*’. Hili lilibainika katika kauli zifuatazo za watafitiwa waliosema, “*andũ ma Kĩrĩnyaga nĩmabũthagio na kũnyararwo mũno*” (Watu wa Kĩrĩnyaga wanadhaliilishwa sana) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 82**). “*magutuaga atĩ wĩ mukĩgu yaani kwĩ na uirano*” (wanaashiria kuwa wewe ni mjinga yaani kuna kudharauriana). “*Ithuĩ turauga turĩ ciana cia Mumbi but we have not been accepted as Kikuyu*” (sisi husema kuwa sisi ni watotot wa Mumbi lakini tunatengwa na kukanwa kama Wakikuyu) (**Rejelea Kiambatisho J, uk. 86**).

Dondoo 6: Tunukuzi kutoka mahojiano:

Nĩ tondũ wa aspect ya stereotyping ta rĩu the other Kikuyus from Mũrang’a Kiambu na Nyeri are thought to have become civilized earlier compared to us from Kĩrĩnyaga. Rĩu tũkoneka ta andũ marĩ thutha, ona rĩmwe nĩukuigwa makiuga twĩ aritu but this is not true no kũnyararwo tũnyarairwo, nĩkio ndionaga bata gwitanĩo na Agĩkũyũ ona kaba njikare ndi Mũkĩrĩnyaga o ũgũo tukinanagio. (kwa sababu ya uendelezaji wa dhana potofu, kwa mfano, wazungumzaji wengine wa Kikikuyu kutoka Mũrang’a Kiambu na Nyeri hudhaniwa kuwa walipata maendeleo au kustaarabika kabla ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Hali hii hutufanya sisi kuonekana kama watu wasioendelea na waliobaki nyuma, wakati mwingine huwa tunarejelewa kama wajinga lakini hilo si la kweli bali ni kutudharau hutudharau tu. Ndiposa hamna haja kutambulishwa na Wakikuyu heri nitambuliwe kama Mũkĩrĩnyaga) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 82**).

Kutokana na kauli hizi, ni dhahiri kuwa ubaguzi unasababishwa na wazungumzaji wengine wa jamiilugha ya Wakikuyu kutoelewa na kuwa na mionoulimwengu finyu na hasa kushikilia mitazamo hasi kuwahuu wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Kwa upande mwingine wazungumzaji hawa hudhalilishwa kwa kuwa wao huonekana kama wasioendelea katika jamii ya Wakikuyu. Kwa mfano, mtafitiwa alisema, “*mwena inĩ wa maendeleo ĩ development andu ma Kĩrĩnyaga nĩmacereirwo mũno makĩrĩngithanĩo na Agĩkũyũ arĩa angĩ and that is why we feel left out ta Agĩkũyũ.*” (Upande wa maendeleo watu wa Kĩrĩnyaga wakilinganishwa na Wakikuyu wengine waliachwa nyuma ndiposa tunahisi kuwa tunabaguliwa kama wanajamii wa jamii ya

Wakikuyu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 82**). Mtafitiwa mmoja mzee mmoja alikuwa na mtazamo ufuatayo kuhusu kubaguliwa kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, alisema;

Dondoo 7: Tunukuzi kutoka mahojiano;

*Mũgĩcũgũ o na kana Mũndia nĩaguaga e 'inferior' mwena inĩ wa lugha na identity yake. Gĩtũmi nĩ gũkorwo atĩ andũ ma Mũrang'a nĩ mendaga gwĩtwa atĩ nĩo Agĩkũyũ mũno, 'the Originals', magakĩgĩa kĩndũ gĩtagwo kamũitĩo, no ma nĩ ati we are all the same na nĩkĩo rĩmwe ũkũigwa makĩnyihia na kwaria tao nĩgũo mabanane. (Mugichugu na Mundia hujihisi kuwa dhalili upande wa lugha na utambulisho wake. Sababu ni kuwa wazungumzaji kutoka Murang'a huwa wanapenda kuringa na kudai kwamba wao ndiyo Wakikuyu sana, wale halisi, hivyo kuingiza maringo, lakini ukweli ni kuwa sote tuko sawa ndiyo sababu wakati mwingine hunyenyekea na kuzungumza kama wao ili wakubalike) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 82**).*

Dondoo hili linaonyesha kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mtazamo hasi kuhusu utambulisho wao kama Wakikuyu kwa sababu kulingana na mtafitiwa kuna ile dhana ya kudhalilishwa kwamba wao sio Wakikuyu. Kwa mfano,

Dondoo 8: Tunukuzi kutoka mahojiano;

Mwena ũrĩa ũngĩ naguo rĩ no marakanwo atĩ tĩ Agĩkũyũ tondũ Agĩkũyũ a Metumi, Gaki na Kabete nĩ maratuhũthia na gũtũnyarara na kuuga atĩ nĩ kwĩringĩrĩria twĩringagĩrĩria tũtũre Agĩkũyũ. Ona wahota kũigua makĩaria tũmemeini makiuga, 'Mũgĩkũyũ nĩ Mũkabete ona ũmuthĩ ũyu tũraria no marauga Mũgĩkũyũ ni Mũgaki nĩ Metumi no Akĩrĩnyaga matigwetagwo'. No o makĩaria rĩ maugaga atĩ ithũĩ tũrĩ ciana cia Gĩkũyũ na Mũmbi tondũ wa mĩhĩrĩga ĩria kenda. (kwa upande mwingine, wao wanakanwa kwamba wao si Wakikuyu kwa sababu Wakikuyu wa Murang'a, Nyeri na Kiambu wana wadharau na kusema kuwa wao huwa wanajilazimisha tu mbali si Wakikuyu. Hata unaweza kusikia wakati wanazungumza redioni wakisema, 'Mkikuyu ni Mukabete (Kiambu) hata sasa hivi tunavyozungumza bado wanasema Mkikuyu ni Mugaki (Nyeri), ni Metumi (Murang'a) bali Wakirinyaga huwa hawatambuliwi'. Lakini wao wanapoongea wao husema kuwa sisi

ni watoto wa Gikuyu na Mumbi kwa sababu ya koo tisa kamilifu (**Rejelea Kiambatisho J, uk. 85**).

Hali hii ya kudhalilishwa na kubaguliwa kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, kama ilivyobainika katika dondoo hizi iliendelezwa katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano katika mahojiano na mtafitiwa mmoja alieleza jinsi alibaguliwa wakati alipokuwa akinunua shamba huko Kiambu. Alidai kuwa hata baada ya kusikilizana na muuzaji na hata kulipa kiasi chote cha pesa walizokubaliana, alirudishiwa pesa zake kwa sababu yeye anatoka Kirinyaga. Alieleza kuwa muuzaji alisema kuwa hatamuuzia ‘mgeni’ mali yake. Mgeni hapa lina maana kwamba muuzaji alimbagua huyo mnunuzi kwa kuwa yeye si Mkikuyu. Hili linadhihirisha hali ya ubaguzi kwa sababu aliyehusika alionekana kuwa na utofauti hata ingawa yeye anajitambua kama Mkikuyu. Pia watafitiwa walidai kuwa wanatengwa katika shughuli za kisiasa ambapo hawapewi nafasi muhimu zilizo na mamlaka ikilinganishwa na Wakikuyu kutoka Kiambu, Murang’ a na Nyeri. Mtafitiwa mmoja alieleza kuwa sababu ya wao kutengwa ni kuwa wao wanaonekana kuwa wachache na lugha yao haina hadhi katika jamii.

Katika utafiti ilidhihirika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mitazamo hasi kwa sababu huwa wanadhaliishwa kutokana na jinsi wanavyozungumza. Watafitiwa wanahisi kwamba wakati mwingi wanapozungumza wao hudhihakiwa na hii ni njia moja ya wao kudhalilishwa. Kwa mfano, kuna wakati wanaambiwa kuwa wanazungumza kama watoto, ni wajinga na hawajaelimika. Kwa mfano, mmoja wa watafitiwa alidai kwamba akiwa shule ya upili rafiki yake kutoka maeneo ya Murang’ a, alikuwa akimtania kila wakati alipokuwa akizungumza, jambo ambalo lilikuwa likimkasirisha na kumuudhi sana. Mtafitiwa huyu aliapa kamwe hawezi kubadilisha jinsi anavyozungumza na kusisitiza kuwa hata ni afadhali azungumze Kiswahili wala sio Kikikuyu.

Pia ilibainika kwamba wanataniwa hasa wanapoenda kufanya biashara au kutembea katika maeneo mengine kama vile Murang’ a, Nyeri au Kiambu. Kwa mfano mzungumzaji mmoja alisema kuwa kuna wakati alikuwa katika mazingira yaliyokuwa na wazungumzaji wengi wa Kikikuyu, alijaribu kuzungumza kama wao lakini utamkaji wake ukasikika kuwa tofauti. Washiriki wenzake walianza kumtania wakisema kuwa anazungumza kama ‘kana’ (mtoto). Hali

hii kulingana na mtafitiwa humfanya mtu kuwa na hisia hasi kwa sababu hapewi heshima na wakati mwingine anayehusika hujidharau. “Mtoto” imetumika kihasi kama dhana ya kuwadunisha wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kwani wanaashiriwa kama watu ambao hawajapevuka. Huu ni udhalilishaji kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ unaotokana na jinsi wanavyozungumza. Wanadhaliwa kwa sababu lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ zimepewa hadhi ya chini na duni zikilinganishwa na lahaja zinazozungumzwa Murang’a, Kiambu na Nyeri (Ruri, keshatajwa). Lugha ni chombo ambacho huwaunganisha na kuwatenganisha au kuwabagua watu katika jamii (Edwards, 2013). Katika utafiti ilidhihirika kuwa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huwaunganisha wazungumzaji wa lahaja hizi mbili kama Wakĩrĩnyaga. Katika utafiti huu, dhana ya “mtoto” imetumika kihasi ilhali kwa kawaida hutumika kwa njia chanya. Hivyo inadhihirika kuwa dhana ya “mtoto” inaweza kuumbwa kwa namna mbalimbali kutokana na maswala tofauti ikiwemo mienendo, mitazamo na tamaduni. Utafiti huu hukupambanua maswala haya kwa ulishughulikia maswala ya mitazamo, hivyo ni dhana ambayo inaweza kutafitiwa zaidi katika isimujamii.

Asilimia 70 ya watafitiwa waliendeleza mitazamo hasi kuhusu makundi ya kijamii ambayo hawangependa kunasibishwa na kutambulishwa nayo. Kati yao ni wale ambao hawakutaka kunasibishwa na jamiilugha ya Wakikuyu kama inavyobainika katika kauli hii;

Dondoo 9: Tunukuzi kutoka mahojiano;

nĩ Akĩrĩnyaga nĩkĩ? Bĩndĩ ciothe njiguaga tugĩtwo ũguo na mũno nĩ Agĩkũyũ aya angĩ. No ithui nĩ twendaga mũno kwĩtania na nao, ĩ Agĩkũyũ tondũ tugaga twĩ ciana cia Gĩkũyũ na Mũmbi ... no nĩwona o matiratutambura ta wenzao, he bata uriku mũndũ atinde akĩringĩrĩria akĩringĩrĩria kwĩ urĩa ũngĩ angĩkorwo ndaramwenda? (kwa nini ni Akĩrĩnyaga. Wakati mwingi nasikia tukirejelewa kama Akĩrĩnyaga hasa na wale Wakikuyu wengine. Tunapenda sana kujitambulisha nao ila wao huwa hawatutambui kama wamoja wao, kuna haja gani mtu kuendelea kujipendekeza kama hamtaki?) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 80).**

Kauli hii inaashiria kuwa watafitiwa wana mtazamo hasi wao kurejelewa kama Wakikuyu kwa sababu wao hukanwa kuwa ni Wakikuyu hata ingawa kwao wanadhani kuwa wamoja wao. Wanakana utambulishaji na jamii hizi kutokana na tofauti za historia na utamaduni wa kikundi

husika. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alisema, “*rĩrĩa ngwaria rĩ, andu aingĩ meciragia atĩ ndĩ Mũembu, naniĩ ngarega mũno tondũ nĩnjũũ ũgũo ti ma, nĩtondũ kũma ndĩ o mũnini nderagwo atĩ kĩhumo gitũ nĩ Gĩkũyũ na Mũmbi. Ũndũire wa Aembu ndiũũ nĩkĩo ndĩrarega gwĩtanio nao.*” (Ninapozungumza, watu hudhani kwamba mimi ni Muembu lakini hilo si kweli, kwa sababu kwa kuzingatia malezi yangu nilielezwa kwamba asili yetu ni Gĩkũyũ na Mũmbi. Utamaduni wa Waembu siujui na ndiposa ninakataa kutambulishwa nao) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 82).**

Asilimia 30 ya watafitiwa wanaeleza kuwa sababu kuu ya kudhaniwa kuwa Waembu ni kwa kuwa nyakati zilizopita, Kirinyaga ilikuwa katika Wilaya ya Embu. Mmoja wa watafitiwa alisema, “*bĩndĩ ya wathani wa nyakerũ rĩ, makĩgaya mĩbaka ya wathani rĩ matiarĩ na umenyo wa ũkuruhanu wa makundi ma andũ na nĩkĩo meciririe andũ ma Kĩrĩnyaga na ma Embu nĩ kĩndũ kĩmwe.*” (wakati wa utawala wa wakoloni, walipokuwa wakigawa majimbo mbalimbali ya kiutawala, hawakuwa na ujuzi fasaha wa utofauti uliopo kati ya jamii hizi na ndiposa walidhania kuwa kuna ukaribu kati ya wazungumzaji wa maeneo ya Kirinyaga na Embu na kuwaweka pamoja) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 81).** Sababu iliyotolewa ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kudhaniwa kuwa ni Waembu ni kwamba watu kutoka Kirinyaga waliendeleza shughuli zote rasmi za serikali, elimu n.k katika jimbo la Embu mpaka wakati Kirinyaga ilipewa hadhi ya kuwa wilaya.

Watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa uelewano kati yao na wazungumzaji wengine wa Kikikuyu ni dhana dhahiri ya mshikamano wa kijamii. Kwa mfano mshiriki mmoja alisema, “*Kĩrĩa gĩtũmaga rũthiomi rũakwa rũkorwo rwĩ na ngũrani na rwa Mũkabete nĩ tondũ rũrĩmĩ rũakwa nĩ rũritũ. O na kũrĩ ũguo ningutaũkĩrũo nĩ tondũ kĩrĩa ndĩraria nĩ kĩmwe na gĩa Gĩkũyũ.*” (Kinacholeta utofauti kati ya lugha yangu na ile ya ‘Mũkabete’ ni kwa sababu ulimi wangu ambao ni mzito. Hata hivyo, kuna uelewano sababu ninachozungumza ni sawa kimaana katika lugha ya Kikikuyu) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 81).** Massamba et al. (2004), wanadai kuwa lafudhi ni sifa ya kimasikizi ya matamshi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji utambulisho fulani kijamii au kieneo. Hii ndiyo sababu wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hupewa utambulisho tofauti na wazungumzaji wengine wa Kikikuyu. Hata hivyo, watafitiwa walieleza kwamba hata ingawa wanazungumza kwa lafudhi tofauti na Wakikuyu wenzao, hii haifai kuwa sababu ya

kuwatenganisha na jamii ya Wakikuyu. Hili lilibainika katika kauli ya mshiriki mmoja aliyesema, “*Rũthiomi rwa Mũndia ni ‘tofauti’ na rwa Mũgĩkũyũ wa Mũrang’a, Kĩambu, no andũ nĩ a mũthingi ũmwe wa Ũgĩkũyũ.*” (Utamkaji wa Mundia ni tofauti na ule wa Mũkũyũ kutoka Mũrang’a na Kĩambu, hata hivyo watu hawa ni wa asili moja ya Kikuyu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 81**).

Kutokana na kutengwa huku, asilimia ya 27 watafitiwa waliendeleza mtazamo hasi kuhusu kuainishwa na hata kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu. Watafitiwa walikataa na kukana kutambulishwa na Wakikuyu na kutaka utambulisho wao kama Wakĩrĩnyaga. Wazungumzaji hawa wanaona lahaja wanayozungumza kama rasilimali na kwamba ni lugha inayoashiria utambulisho wao kama wanajamii. Lugha ambayo wanadai inawatambulisha kama Wakĩrĩnyaga ni Gĩkĩrĩnyaga. Pili, mbali na kuwa na lugha inayowatambulisha kama Wakĩrĩnyaga, wanaamini kuwa wana utamaduni tofauti na ule wa Wakikuyu na wangetaka kurejelewa kama Wakĩrĩnyaga kwa sababu lugha na utamaduni wao unadidimia hasa kwa sababu lugha zao, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ zinadhililishwa na hazijapewa hadhi.

Ili kuthibitisha mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ sio Wakikuyu mbali Wakĩrĩnyaga, walitoa madai kuwa mfumo wao wa kupeana majina una utofauti na ule wa jamii ya Wakikuyu. Kwa kulinganisha majina yanayotumika baina yao na Wakikuyu, wanadai kuwa watu Wakĩrĩnyaga wanapenda sana kutumia majina ya wanyama na majina yanayoashiria heshima hasa kwa wazee. Hata ingawa wanahisi kuwa hili linawapa nafasi ya wao kutambulishwa kama Wakĩrĩnyaga kuna ukinzani unaotokea kwa sababu inadhihirika kuwa wanaendeleza kaida sawa na zile za kupeana majina katika jamiilugha ya Wakikuyu. Watafitiwa wanakubali kuwa wanafuata kaida anazoeleza Kenyatta, (keshatajwa) za mtoto wa kwanza wa kiume/ kike hupewa jina la baba/ mama ya mzazi wa kiume ilhali wa mtoto wa pili wa kiume/ kike hupewa jina la baba/ mama ya mzazi wa kike mtawalia.

Utambulisho wa mtu au jamii huwa mchakato ambao huhusisha vibainishi vingi vikiwemo lugha, utamaduni, mila na desturi (Scherer & Giles, 1979). Asilimia 27 ya watafitiwa, ambao wana mtazamo kuwa ‘Gĩkĩrĩnyaga’ huwatambulisha wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ katika maeneo ya Kirinyaga kwa ujumla na wanasisitiza kwamba lugha hii, Gĩkĩrĩnyaga, ina upekee na

hutofautiana na Kikikuyu. Ili kuthibitisha tofauti zilizoko kati ya Gĩkĩrĩnyaga na Kikikuyu, watafitiwa walitoa baadhi ya misamiati. Kwa mfano,

| <u>Gĩkĩrĩnyaga</u> | <u>Kikikuyu</u> |
|--------------------|-----------------------------|
| <i>Wagui</i> | <i>guka</i> (babu) |
| <i>Kuminjia</i> | <i>kuhinga</i> (kufunga) |
| <i>Kuracukia</i> | <i>kuhingura</i> (kufungua) |
| <i>Ithĩga</i> | <i>ihiga</i> (mawe) |
| <i>Arĩ</i> | <i>aca</i> (hapana) |

Kwa kuzingatia mifano hii na mingine, watafitiwa walikuwa wanajaribu kuisistiza kwamba lugha yao ya Gĩkĩrĩnyaga ni tofauti na Kikikuyu na hivyo basi wanapaswa kutambuliwa kama jamii tofauti na ile ya Wakikuyu. Hata hivyo, tofauti hizi ni za kilahaja (Mutahi, 1977), na wala hazina mashiko ya kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanapaswa kupewa utambulisho wao kama kundi jamii tofauti na ile ya Wakikuyu.

Watafitiwa wana mtazamo kuwa lugha ni ala muhimu katika utambulisho wa mzungumzaji. Ili kufanikisha utambulishaji wao kama Wakĩrĩnyaga, baadhi ya watafitiwa wana mtazamo kuwa lazima watoto wafunzwe lugha ya Gĩkĩrĩnyaga shuleni. Hata hivyo, hili haliwezi kufanikishwa kwa sababu hakuna vitabu vyovyote ambavyo vimeandikwa kwa Kĩndia wala Kĩgĩchũgũ. Mtafitiwa mmoja alisema, “*ona tũkiugaga atĩ ciana citũ cithome rũthiomi rũrũ rwitũ, no mũhaka mũtaratara ya kũandika mabuku marĩa mangĩbũthĩrwo ãthondekwo tondũ maingĩ maandĩkĩtwo na Gĩkũyũ.*” (hata kama tungependa watoto wetu wafunzwe hii lugha yetu, ni lazima taratibu za kuandika vitabu vitakavyotumiwa ziwewe sababu vingi vimeandikwa kwa Kikikuyu”) (**Rejelea Kiambatisho 1, uk. 84**). Suala lingine ambalo lilibainika ni kwamba, hakuna makubaliano ni lahaja gani kati ya Kĩndia na Kĩgĩchũgũ itatumika katika uandishi wa vitabu hizi. Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hazijaandikiwa othografia hivyo itakuwa vigumu kufundisha lugha hizi shuleni na ndiposa watafitiwa walikuwa wanashinikiza kuwa wazazi wachukue jukumu hilo katika mazingira ya nyumbani.

Kulingana na mtafitiwa mmoja, wazungumzaji wa Kĩndia hurejelewa kama “*ndia ndiitu*” (Wandia wajinga). Hali hii ya kudhalilishwa huendelezwa na Wakikuyu na hata Wagichugu.

Mtafitiwa huyu alidai kwamba, “*rĩrĩa tũgwĩtwo ndia nditũ rĩ, tĩ atĩ tũrĩ aritũ no nĩ tondũ wa utana witũ*” (tunaporejelewa kama ‘ndia nditu’, haimaanishi kwamba sisi ni wajinga bali ni kwa sababu ya ukarimu wetu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 83**). Kwa mtazamo wake, katika jamii ya Wakikuyu, Wandia ndiyo watu wakarimu sana na walio na utu kwani hawabagui yeyote yule. Aliendelea kusema kuwa kutokana na ukarimu huu, Wandia wameuza mashamba yao kwa Wakikuyu wenzao na hata makabila mbalimbali kutokana na ukarimu wao. Kulingana na mtafitiwa huyu, kudhalilishwa kwa njia yoyote ile sio sababu tosha ya kuukana utambulisho wake na jamiilugha ya Wakikuyu. Muhimu katika utambulisho wa kikundi fulani cha kijamii ni kuwa washiriki wanazingatia utamaduni, mila, desturi, tajriba na historia sawa. Kwa mtazamo wake, yeye kama zao la Gĩkũyũ na Mũmbi, anazingatia na kufuata utamaduni wa Wakikuyu na hivyo anafaa kutambulishwa kama Mkikuyu.

Hali kadhalika, mtafiti alitaka kuelewa mtazamo wao kuhusu jinsi wangependelea kurejelewa na wazungumzaji wengine, hasa, wa Kikikuyu kuhusiana na utambulisho wao wa kijamii. Asilimia 70 ya watafitiwa walisema kuwa wao wangetaka kutambulishwa kama Wakikuyu. Madai haya yaliibuka katika mahojiano ya mtafitiwa mmoja ambaye alisema, “*nĩ njũ ndĩ Mũgĩkũyũ na angĩkorwo matinyonaga ta ndĩ Mũgĩkũyũ rĩ, no nyende mamenye atĩ hakwa ndĩ Mũgĩkũyũ tondũ ndikĩrĩ Mũemba kana Mũmeru tondũ ũndũire wao ti ũmwe na ũrĩa nũmagĩrĩra na nĩgũo wa Mũgĩkũyũ.*” (mimi ni Mkikuyu na kama hawanitambui kama Mkikuyu, ningependa waelewi kwamba kwangu mimi ni Mkikuyu sababu siwezi kutambulishwa na Waemba wala Wameru sababu utamaduni wao ni tofauti na ule ambao ninaofuata, wa Wakikuyu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 84**).

Asilimia 20 ya watafitiwa walidai kwamba, wao kuainishwa na kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu ni kutokana na sababu za kisiasa. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alidai kwamba Kenyatta ndiye alisababisha wao kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu kwa sababu alitaka wafuasi katika uongozi wake. Alisema, “*Kenyatta nĩwe watũmire twĩtwo Agĩkũyũ nĩgũo athĩe agĩĩtaga na Gĩkũyũ gĩake...warĩ mũtaratara wake ahote gwithana*”. (Kenyatta ndiye alisababisha sisi kutambulishwa kama Wakikuyu ili aweze kujivuna na Wakikuyu kama watu wake, kisiasa... ilikuwa ni mfumo wa kumsaidia kutawala) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 81**). Ni wazi kuwa katika

nchi ya Kenya wanasiasa hutegemea wingi wa wafuasi au wapiga kura kutokana kwa kabila lao na ndiposa watafitiwa wanaamini kuwa Kenyatta alitaka Wakikuyu waongezeke kwa wingi ili aweze kupata mamlaka.

Kila jamii hutofautiana katika utaratibu wa kupeana majina. Majina huwa sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii husika. Jina ni utambulisho na utamaduni wa binadamu katika jamii mbalimbali. Mfumo wa kupeana majina ulibainika kuwa muhimu katika kuendeleza utambulisho wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Watafitiwa walieleza kuwa, katika shughuli za kupeana majina, wanazingatia mfumo uliokubalika katika jamiilugha ya Wakikuyu. Mtoto wa kwanza, wa kike au kiume, anapewa jina kutoka upande wa baba yake na wa pili upande wa mama (Kenyatta, 1938). Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanabadilisha jina lile kutokana na hali au mazingira fulani kama njia ya heshima. Wanaamini kuwa kila mtu ana majina zaidi ya moja ambayo huchaguliwa kupewa mtoto ili kuendeleza heshima. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alisema kuwa alistahili kupewa jina Munene lakini kwa sababu watoto waliotangulia kuzaliwa na kupewa jina hilo walikufa, wazazi wake walimbadilishia jina na kumwita Gitari. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa ujinaishaji kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huzingatia sifa ya mhusika, kitu au hata kazi ambayo alikuwa anafanya k.m Mureithi (mfugaji wa mifugo), Murĩmi (mkulima) na kadhalika.

Katika kila jamii kuna mfumo wa kiutamaduni ambao huzingatiwa katika masuala ya ndoa. Katika utafiti ilibainika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanatambua na kuendeleza mfumo wa ndoa kama Wakikuyu wengine. Kwa mfano, “*Kĩũgĩkũyũ nĩ kũrĩ mũtarara ĩrĩa ĩrũmagĩrĩrwo rĩrĩa mwanake na mũirĩtu marena kũhikania kũuma kũhanda ĩthĩgĩ kwa mũirĩtu ngĩnya kũracia, ĩrĩa ona ithũĩ ta Agĩchũgũ na Andia tũrũmagĩrĩa.*” (Katika utamaduni wa Wakikuyu kuna hatua ambazo zinapaswa kufuatwa wakati mvulana na msichana wanapotaka kuoana ikiwemo wakati wa kujua kwa msichana ‘*kuhanda ithĩgĩ,*’ mpaka kutoa mahari (*ruracio*) na ndiyo wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huzingatia) TY. “*Mwanake enda kuũhikania rĩ Gĩgĩkũyũ no mũhaka aracie kwa mũirĩtu na rĩracio rwa Mũgĩkũyũ rutithiraga*” (Kijana anapoamua kuoahiliwa ni lazima kulingana na utamaduni wa Kikuyu atoe mahari kwa msichana...na ulipaji wa mahari huendelezwa kwa kipindi kirefu) (**Rejelea Kiambatisho I, uk.**

80). Watafitiwa hawa na wengine wanajijengea silka za utambulisho na jamii ya Wakikuyu kwa kuwa wanazingatia utamaduni katika masuala ya kindoa na ule unaozingatiwa katika jamii ya Wakikuyu.

Kwa kuhitimisha, kutokana na matokeo ya utafiti, ni bayana kwamba wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana ufahamu wa asili na utambulisho wao kama wanajamii wa jamii ya Wakikuyu kwa kuwa wao ni zao la Gikuyu na Mumbi. Zaidi ya kuwa na ule ufahamu, wanakubali kuwa wanafuata na kuzingatia taratibu nyingi za kiutamaduni kama vile za kindoa, kupeana majina ya watoto, majina ya ukoo n.k zinazodumishwa na Wakikuyu wengine na hivyo kuwapa nafasi ya kujitambulisha na jamii ya Wakikuyu. Watafitiwa walisisitiza kwamba utambulisho wa kijamii wa mtu binafsi au kundi la jamii hutokana na utamaduni wa jamii husika bali sio lugha tu. Lugha ya wazungumzaji wa jamii moja hutofautiana lakini mila, desturi, utamaduni huwa sawa. Ukubalifu wa mifumo mbalimbali ya kijamii na asilimia tisini ya watafitiwa ina maana kwamba wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana uelewa fasaha wa mifumo hii inavyoendeleza mshikamano na umoja kwa wanajamii wa jamii ya Wakikuyu.

4.3 Matumizi ya Lugha

Matumizi ya lugha katika ufafanuzi wa utambulisho wa kijamii ulizingatiwa katika utathmini wa ufanano na utofauti uliodhihirika katika usemi wa watafitiwa katika miktadha tofauti ikiwemo nyumbani, sokoni na kadhalika. Kabla ya kutathmini michakato ya ufanano na utofauti iliyodhihirika wakati wa matumizi ya lugha, ni muhimu kuelewa jinsi wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanatumia lugha wanapotangamana na wazungumzaji wengine wa lugha ya Kikikuyu.

4.3.1 Matumizi ya Lugha ya Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ

Kwanza, mtafiti alitaka kuelewa lugha ambayo wanatumia wakati wanawasiliana na wenzao wanaozungumza lugha ya Kikikuyu. Watafitiwa walieleza kwamba kwa kawaida huwa wanatumia lugha zao ila kuna wakati mwingine inawabidi kuchanganya ndimi na kuzungumza lugha ya Kiswahili. Crystal (1969), anasema kuwa mzungumzaji hawezi kutumia mtindo mmoja wa mazungumzo akizungumza na makundi tofauti ya watu. Utafiti ulibainisha kuwa watafitiwa walichanganya na kubadili ndimi hasa walipokuwa wakizungumza na wasemaji wa ‘*Kĩhaha*’

ambao ni wale Wakikuyu kutoka maeneo ya Nyeri, Murang'a na Kiambu. Katika matumizi ya lugha mzungumzaji huzungumza kwa kuzingatia hadhira ya washiriki katika mazungumzo (Crystal, 1969). Wakikuyu wengine ambao hawazungumzi lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanarejelewa kama 'wahaha' ama 'wahihĩ' kwa sababu ya matumizi ya sauti /h/. Sauti /h/ haitumiwi na wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ na badala yake wao hutumia sauti /b/ ambayo hutamkwa /β/ kama inavyoashiriwa katika jedwali ifutayo;

Jedwali 4: Konsonanti za Lugha ya Kikikuyu

| Mahali na Namna ya kutamka | Midomo | Meno+ulimi | Ufizi | Kaakaa+ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koo |
|----------------------------|------------------------|------------|---------------------|------------------------|-------------|---------------------|-------|
| Vipasuo | / ^m b/ (mb) | | /t/ (t) /nd/(nd) | | | /k/ (k) /ŋ/ (ng) | |
| Vikwamizo | /β/ (b) | /ð/ (th) | /s/ | /f/(c) | | /ɣ/ (g) | h (h) |
| Kipasuo-kwamizo | | | | / ⁿ dʒ/(nj) | | | |
| Nazali/Ving'ong'o | /m/(m) | | /n/ (n) | | /ɲ/ (ny) | /ŋ/ (ng') | |
| Kimadende | | | /r/ (r) | | | | |
| Viyeyusho | w/ (w) | | | | /j/ (y) | | |

Kulingana na Iribemwangi (2016), tofauti kuu kati ya lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ na lahaja zingine za Kikikuyu ni kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hutumia fonimu /β/ ilhali Lahaja zingine za Kikikuyu hutumia fonimu /h/. Pia anadai kuwa lahaja za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hazina fonimu /f/ na /tʃ/ na badala yake ni fonimu /s/. Kuna uelewano wa wazungumzaji kwani hizi ni tofauti za kilahaja zinazotokana na maeneo ya kijiografia ya wazungumzaji. Kwa mfano;

| <u>Kĩndia na Kĩgĩchũgũ</u> | <u>Kikikuyu</u> | <u>Kiswahili</u> |
|----------------------------|-----------------|------------------|
| <i>Kaβora</i> | <i>Kahora</i> | Polepole |
| <i>Maβeni</i> | <i>Maheni</i> | Uwongo |

| | | |
|---------------|---------------|-----------|
| <i>Kuβĩa</i> | <i>Kuhĩa</i> | Kuchomeka |
| <i>Iβenya</i> | <i>Ihenya</i> | Mbio |
| <i>Mbeβo</i> | <i>Heho</i> | Baridi |
| <i>Siana</i> | <i>Ciana</i> | Watoto |
| <i>Isembe</i> | <i>Icembe</i> | Jembe |

Matumizi ya lugha Kiswahili yalidhihirika katika mazungumzo baina ya wazungumzaji wa Kĩndia, Kĩgĩchũgũ na wale wa Kikikuyu Hali hii ya kuchanganya ndimi ilibainika kutokea wakati watafitiwa walizungumza na mzungumzaji ambaye ni mgeni katika maeneo ya Mwea, sababu wakati mwingi huwa hawana ufasaha wa lahaja husika, hasa Kĩgĩchũgũ. Wale ambao wameishi katika maeneo haya kwa muda mrefu huwa hawana matatizo kuelewana. Hata hivyo, ilibainika kuwa uchanganyaji msimbo huweza kuendelezwa kwa kiwango kikubwa na wazungumzaji wa Kĩndia wala sio wa Kĩgĩchũgũ. Hili linadhihirika kutoka mtazamo wa mtafitiwa aliyesema, “*gũtirĩ kĩndũ makabeo hau hata nitawaambia direct wasahau kabisa ciothe cigathie*” (Hakuna kitu watapewa hao hata nitawambia wasahau kabisa zote zitaenda). Mzungumzaji anajaribu kuonyesha hisia zake za kuchukizwa.

Hali ya kuchanganya ndimi pia iliendelezwa wakati wazazi walikuwa wakizungumza na watoto wao. Watafitiwa wanadai kwamba wakati mwingi watoto wako shuleni ambako huzungumza Kiswahili na Kiingereza kwa kuwa hizo ndizo lugha zitakazowafaidi shuleni. Hili linawiana na mtazamo wa Gachiri (2009), anayedai kuwa nchini Kenya kuna msisitizo wa kiwango cha juu cha matumizi ya Kiingereza na Kiswahili katika mfumo wa elimu huku lugha za mama zikipuuzwa. Kutokana na hali hii, watoto hawana muda wa kujifunza lahaja zao za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Asilimia 80 ya watafitiwa wazee walikuwa na hisia kali kuhusu hali hii ya kizazi cha kisasa kuzungumza na watoto wao kwa lugha ya Kiswahili badala yao kuwafunza lugha yao ya mama. Wazee walikuwa na madai kuwa kwa kuipa lugha ya Kiswahili nafasi ya kwanza, lugha ya Kikikuyu inaendelea kudidimia. Ili kubadilisha hali hii walipendekeza ufundishwaji wa lugha ya Kikuyu uzingatiwe na uendelezwe kwa watoto kama ilivyokuwa katika masomo ya awali iliyofunza ‘*Gikũyũ gĩa TKK*’. Kwa kufundisha Kikuyu shuleni watoto wa umri mdogo hasa katika masomo ya chekechea watajua lugha yao ya Kikikuyu na kusaidia kutofifia kwa lugha hii ambayo

watafitiwa wengi wazee walikubali inaelekea kufifia. Pia walikuwa na mtazamo kuwa lugha ya mama ni muhimu katika kuendeleza utamaduni wa jamii yoyote ile. Hili linawiana na maoni ya Muaka (2009), anaposema kuwa watu wengi wana mwelekeo chanya kuhusu lugha za mama kama vyombo mwafaka vya kuhifadhi utamaduni na historia za jamii zao na kuzipitisha kwa vizazi vijavyo. Lugha inapoteza uamilifu wake kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa wanajamii, kuna uwezekano kuwa itatoweka. Watafitiwa waliokuwa na mtazamo kuwa ‘*Gĩkĩrĩnyaga*’ ndiyo lugha yao, walipendekeza na kusisitiza kuwa ndiyo inapaswa kupitishwa kwa watoto wao katika mashule wala sio Kikikuyu. Hata hivyo, kwa kuwa vitabu vingi vimeandikwa kwa Kikuyu sanifu, waliokuwa na mtazamo huu walitoa mapendekezo ya uchapishaji wa vitabu kwa lugha yao, *Gĩkĩrĩnyaga*.

Zaidi ya hayo, katika matumizi ya lugha kati ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hakukuwa na haja ya ubadilishaji usemi kwa sababu walikuwa na mtazamo kuwa hakuna utofauti mkubwa kati yao kwani wanatumia lafudhi sawa. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alisema, “*Andia na Agĩchũgũ nĩ Akĩrĩnyaga na maragia ũndũ umwe na gũtirĩ hĩndĩ ukaigua ũmwe witu akiuga aĩ ndarraigwa kĩrĩa mwenzake arauga mĩkarĩre na mĩtugo itũ nĩ ĩmwe*”. (Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni Wakĩrĩnyaga na huzungumza kwa njia sawa na hakuna wakati wowote utasikia madai ya kuwa hatuelewani... mila na desturi zetu ni sawa) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 83**). Kulingana na maoni ya watafitiwa, kinachofanya Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuwa tofauti ni kuwa wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ huzungumza kwa kutumia toni ya juu sana wakilinganishwa na wazungumzaji wa Kĩndia.

Utafiti ulibainisha kwamba asilimia 35.7 ya vijana na rika la kati ambao wamezaliwa katika maeneo haya ya Mwea wameunda kijilugha chao ambacho wanakitambulisha kama ‘*Kĩmwea*’, ‘*Kĩthuguthugu*’. Kulingana nao, Kimwea ni mchanganyiko wa Kĩndia, Kĩgĩchũgũ na *Kĩhaha* hata ingawa Kĩndia kinatawala zaidi kutokana na sababu kuwa wazungumzaji wa Kĩndia ndiyo wengi kuliko wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ katika eneo hili la Mwea. Wengi wanaotumia *Kĩmwea* wanadai kwamba, kijilugha hiki kinarahisisha mawasiliano kati ya wazungumzaji na kuendeleza mshikamano kati yao. Kati ya vijana ambao wanadai kwamba wanazungumza *Kĩmwea* ni wale ambao wamezaliwa katika eneo la Mwea kwani wanaamini kuwa wanaozungumza Kĩndia na

Kĩgĩchũgũ ni wazee na wale ambao wanaoishi katika maeneo mbunge ya Ndia na Gichugu. Ilibainika kwamba suala la vijana kuwa na namna yao ya kuzungumza ilitokana na maingiliano ya kindoa, ndoa baina ya Wandia, Wagichugu na Wakikuyu.

Uundaji wa misimbo hii mipya kati ya vijana unawiana na maoni ya Eckert (2003), anapodai kwamba, mbali na kundi la vijana kuhusika na matumizi ya lugha nyingi katika jamii, sifa nyingine kuu ya vijana ulimwenguni ni kutaka kufanya uvumbuzi mwingi katika matumizi ya lugha hadi kiwango cha kuziunda lugha na misimbo mipya na kujiundia utambulisho wao katika jamii. Hali hii ya vijana kujiundia vijilugha na misimbo mbalimbali inawiana na mawazo ya Thornborrow (keshatajwa), anaposema kuwa vikundi vya kijamii hutmia lugha kama njia ya kujitambulisha kama washiriki wa kundi la jamii moja na hili huunda dhana ya makundi “ndani” na “nje”. Hivyo, ni dhahiri kuwa vijana watumia lugha yao kujiundia kundi lao “ndani” linalowatambulisha kama kikundi cha kijamii kilicho tofauti na makundi mengine ya “nje.” Wanatumia ‘*Kĩmwea*’/‘*Kĩthuguthugu*’ kama alama ya ushirika wao kama wanachama wa kikundi cha kijamii.

4.3.2 Michakato ya Kiisimu ya Kiukaribiano

Giles (2016), anadai kwamba mzungumzaji wa kundi fulani la kijamii hupunguza au kusesitiza mipaka baina yake na wazungumzaji wengine wa kundi hilo kwa nia ya maafikiano kwa jinsi anavyotumia lugha. Maafikiano haya huendelezwa kwa minanjili ya kudumisha uhusiano baina ya wazungumzaji. Anaendelea kusema kuwa maafikiano haya huhusisha ubadilishaji wa usemi unaomtambulisha mzungumzaji kama mwanajamii wa kundi husika. Mabadiliko haya huweza kutokea bila hiara ya mzungumzaji hata ingawa kuna wakati yanatokea kwa hiari kama ilivyobainika katika utafiti huu. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alidai kuwa anazungumza Kikikuyu kwa hiari kwa sababu anataka kumfurahisha mshiriki mwenzake katika mazungumzo. Kuna uwezekano mkubwa wa kuathiriana katika vipengele mbalimbali vya kiisimu kunapokuwa na mtagusano wa lugha katika jamii, hata kama wanaohusika kimazungumzo ni wanajamii wa lugha moja (Giles, 1991). Utafiti huu ulinuia kuchunguza michakato ya kiisimu iliyoendelezwa katika mazungumzo ya watafitiwa, na kuiweka bayana michakato hiyo ya kiisimu kati ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ katika miktadha mbalimbali.

Katika utafiti ilibainika kwamba watafitiwa wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ waliendeleza ukaribiano wa ufanano na wazungumzaji wa Kikikuyu kwa kuingiza sauti kama vile sauti /h/ katika uzungumzaji wao. Sauti /h/ haitumiwi na wazungumzaji wa Kĩndia au Kĩgĩchũgũ na badala yake hutumia sauti /b/. Hata hivyo, mtafitiwa mmoja wa Kĩndia, kutokana na mazingira alimoishi kwa muda mrefu akiwa kijana alipata kuathirika na kuanza kuzungumza tofauti na wazungumzaji wengine wa Kĩndia. Mtafitiwa huyu aliendeleza matumizi ya /h/ badala ya /b/ kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo baina yake na mzungumzaji wa Kikikuyu,

Mz1: *ũhoro, kaĩ wacokire rĩ?*

Mz2: *mwega, ndacokire o Kiumia*

Mz1: *nĩkĩĩ wagĩtũreheire*

Mz2: *ndokire o ũguo...Wa Mose nĩ ũmwĩrĩga? Nĩ ahonire?*

Mz1: *ah! ucio ahonire na agĩcoka wĩra*

Kwa kawaida mzungumzaji huyu angetamka kama ifautavyo;

Mz1: *ũboro, kaĩ wacokire rĩ?*

Mz2: *mwega, ndacokire o Kiumia*

Mz1: *nĩkĩĩ wagĩtũrebeire*

Mz2: *ndokire o ũguo...Wa Mose nĩ ũmwĩrĩga? Nĩ abonire?*

Mz1: *ah! ucio abonire na agĩcoka wĩra*

Mz1: *habari kwani urirudi lini?*

Mz2: *Mzuri, nilirudi Jumapili*

Mz1: *ulituletea nini?*

Mz2: *sikuja na chochote...Mmeonana na Wa Mose? Alipona?*

Mz1: *Ah! Huyo alipona na akarudi kazini*

(Rejelea Kiambatisho L, uk. 89).

Kwa mujibu wa nadharia ya ukaribiano, inapotokea jamiilugha mbili zinazokaribiana kimaeneo kuendeleza mazungumzo na kuna mabadiliko ya kiusemi kutoka lugha moja hadi lugha nyingine basi hili linaashiria kwamba kuna mfanano. Mfanano huu unaweza kuwa wa juu au chini

kwa kutegemea mzungumzaji anabadili lahaja yake kutoka kwa isiyo sanifu hadi ile iliyo sanifu na kinyume chake. Mfanano wa juu huhusisha kubadili lugha au lahaja iliyo na hadhi na ile isiyo na hadhi. Mzungumzaji anabadili usemi na kusisitiza kuzungumza lugha ya Kikikuyu sanifu ilhali yeye ni mzungumzaji Kĩndia, lahaja inayochukuliwa kuwa haina hadhi (Ruri, 2011), basi huu unaashiria mfanano wa juu. Wakati mwingine wanoendeleza mfanano wa juu huchukulia kuwa lugha au lahaja yao ni duni na ili kukubalika anazungumza ile iliyo sanifu. Kwa upande mwingine, mzungumzaji wa lugha iliyo na hadhi anapotilia mkazo uzungumzaji wa lugha au lahaja isiyo na hadhi basi anaendeleza mfanano wa chini.

Katika mfano kati ya mzungumzaji (Mz1) na (Mz2) (katika Uk.50), unahusisha mzungumzaji wa Kĩndia na wa Kikikuyu, mfanano wa juu unaendelezwa na mzungumzaji wa Kĩgĩchũgũ ambaye anabadili utamkaji wa sauti /b/ na badala yake anatumia sauti /h/ ambayo hutumika katika Kikikuyu sanifu. Sauti hizi zinabadilishana nafasi bila kubadili maana ya neno, uhusiano unaojulikana kama mpishano huru. Mpishano huru ni uhusiano wa fonimu mbili tofauti kubadilishana nafasi bila kubadili maana ya maneno husika. Sauti /h/ na /b/ hazipo katika ule uhusiano wa kiutoano, yaani, zote zinaweza kutumika katika mazingira sawa kwenye neno bila kubadili maana. Mtafiti alitaka kujua sababu ya mtafitiwa kuendeleza matumizi ya sauti /h/ na kama huwa anaitumia kila wakati alipokuwa akizungumza. Mtafitiwa alieleza kwamba wakati mwingi huwa anatumia sauti /h/ badala ya /b/ kwa sababu ameishi na kufanya kazi na Wakikuyu wengi mpaka akajikuta ana mazoea ya kutumia ile sauti. Alisema, “*maingĩ ndĩkoraga ngĩaria ta ahaha nĩ tondũ wa gũikarania nao. Nĩwamenya gũkũ Gathigiriri ahaha nĩ aingĩ mũno na o ũrĩa tũraikarania nao, twĩkoraga nĩ tũtahirwo na tũkaria o tao*” (wakati mwingi huwa najikuta nazungumza kama Wakikuyu kwa sababu ya athari za kuishi pamoja nao. Unajua huku Gathigiriri Wakikuyu ni wengi mno na jinsi tunaendelea kuishi pamoja hujikuta tunazungumza kama wao) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 84)**. Anaendelea kusema kuwa ili kuwe na umoja na mshikamano kati yao kama wakaazi wa maeneo haya, wanabiidika kubadili usemi wao ili kufanana na washiriki wengine ambao ndiyo wengi hasa katika mazungumzo.

Katika mazungumzo kati ya wazee wawili, mzungumzaji wa Kĩndia na Kikikuyu, mfanano unatokea kama inavyoashiriwa katika mfano huu; “*Ūboro ũcio ndũrangenia ona banini akorwo*

mararĩ ega maragĩte kũheo nĩkĩ? Kaĩ marĩ kũ mũthee agĩgakinya kũgaya na kũheana mũgũnda ũcio gũtirĩ kĩndũ makaheo” (Habari hiyo hainifurahishi hata kidogo...kama walikuwa wazuri walikosa kupewa kwa nini? Kwani walikuwa wapi mzee alipoamua kugawa na kupeana shamba hiyo). Katika kauli hii, mzungumzaji huyu wa Kĩndia anabadili sauti /b/ na badala yake anasisitiza kutumia /h/. Mtafitiwa anajaribu kupunguza utofauti wa kiisimu kati yake na anayezungumza naye ili kupitisha ujumbe wake kwa namna ambayo itaeleweka kwa ufasaha. Hili linawiana na maoni ya Giles (1975), anaposema kuwa mshiriki wa kikundi fulani cha kijamii hupunguza mipaka baina yake na washiriki wengine wa kundi hilo kwa nia ya kuafikiana.

Hali ya mwachano ilidhihirika katika mazungumzo ya vijana wawili ambao walidai kwamba lugha yao ya kwanza ni Kĩndia. Katika mazungumzo ya watafitiwa hawa, ilibainika kuwa mtafitiwa mmoja alikuwa anazungumza Kikikuyu wala sio Kĩndia kama inavyoashiria katika mfano huu,

Mz3: *Kũi, wathiĩ kũ*

Mz4: *gũtaha maĩ harĩa*

Mz3: *kaĩ kwanyu gũtari na maĩ*

Mz4: *gwitũ nĩ mahingirwo*

Mz3: *mũkĩbingĩrwo maĩ nĩkĩ? kaĩ mũtarĩbaga*

Mz4: *nĩtũrĩhaga no anga mathĩna mangĩ*

Mz3: *na ngũrie ĩ, kaĩ Mũthoni wanyu athire kũ?*

Mz4: *Mũthoni athire kibarua Nairobi*

Mz3: *Ngai! mabeni wee*

Mz4: *atĩ maheni. Kaĩ atakũĩririre na nĩ mũratagwo?*

Mz3: *Kui, unaenda wapi?*

Mz4: *kuchota maji pale*

Mz3: *kwani kwenu hakuna maji*

Mz4: *kwetu maji yalifungwa*

Mz3: *mlifungwiwa kwa nini? Kwani huwa hamlipi*

Mz4: tunalipa labda ni sababu zingine

Mz3: na nikuulize, kwani Muthoni wenu alienda wapi?

Mz4: Muthoni alienda kibarua Nairobi

Mz3: uwongo huo

Mz4: ati uwongo. Kwani hakukuambia na ni rafiki yako?

(Rejelea Kiambatisho L, uk. 89).

Katika mfano huu, mtafitiwa anazungumza kwa kutumia sauti /h/ ambayo huwa ni sanifu na pia lafudhi yake inasikika kuwa imebadilika ikilinganishwa na ile ya rafiki yake. Kwa minajili ya nadharia ya ukaribiano ya Giles, wakati mzungumzaji anawacha kuzungumza lugha au lahaja yake na kuanza kuzungumza ile iliyo sanifu basi hiyo ni aina ya mwachano wa juu kwa kuwa anasisitiza matumizi ya sauti /h/ambayo hutumika katika Kikikuyu sanifu. Mtafiti alitaka kujua sababu mtafitiwa alikuwa anazungumza kwa namna hii na aligundua kwamba mtafitiwa ameishi na Wakikuyu wengine ambao anaamini wanazungumza Kikikuyu sanifu kwa muda mrefu. Hii ni kutokana na sababu kuwa wazazi wake wameishi kwa muda mrefu katika maeneo ya Nyeri kikazi. Ni bayana kwamba kutokana na mtafitiwa kuishi katika mazingira haya, ilimbidi kubadili na kuzungumza kama wakaazi wa maeneo hayo ili kukubalika na kujihisi kama mmoja wao.

Kwa upande mwingine, inapotokea kwamba mzungumzaji anaendelea kutumia na kudumisha lugha yake bila kubadili kufanana na ile ya mshiriki wake katika mazungumzo basi mazingira kama hayo yanaonyesha kwamba kuna mwachano au utofauti. Katika mfano, mazungumzo kati ya Mz3 na Mz4, kati ya marafiki wawili, inabainika kwamba mtafitiwa Mz3 anasisitiza kuzungumza Kĩndia bila kubadili sauti /h/ kufanana na rafiki yake. Sababu yake ni kuwa anapenda kuzungumza lugha yake na hiki ni kipengee kinachomsaidia kuendeleza utambulisho wake na kikundi cha kijamii cha Wakĩrĩnyaga. Katika utafiti mwachano katika mazungumzo ulidhihirika pia katika mazungumzo baina ya muuzaji na mnunuzi katika muktadha wa duka kama inavyoashiriwa katika mfano ufuatao;

Mz8: *wĩmwega, tahe uyu tamu*

Mz9: *ũmwega weu, atĩ ũrenda ngube kĩ?*

Mz8: *arenda tamu, kajoice gaka*

Mz9: *mwana! Thaa ici na mbebo*

Mz8: *atĩ heho, we mũhe nĩ thĩna wake*

Mz9: *thĩna wake! Aca! tĩ thĩna wa mwana*

Mz8: habari, hebu mpe huyu tamu

Mz9: habari yako, ati unataka nikupatie nini?

Mz8: anataka tamu, hako kajuice

Mz9: mtoto! Saa hii na baridi

Mz8: ati baridi! Wewe mpe ni shauri yake

Mz9: shauri yake! Hapana! sio shauri ya mtoto

(Rejelea Kiambatisho L, uk. 91).

Katika mazungumzo haya, inabainika kuwa washiriki wanasisitiza na kuendeleza mwachano au utofauti. Hali hii kama anavyodai Giles hutokea wakati mzungumzaji yeyote anataka kudumisha utambulisho wake na kundi lake la kijamii. Mtafitiwa alidai kuwa yeye haoni haja ya kubadilisha kwa sababu wanaelewana, tofauti ni sauti /b/ na /h/ ambazo hutumika katika mazingira sawa bila kubadili maana ya neno husika yaani mpishano huru. Udumishaji wa utambulisho na kundi la kijamii mahususi pia linaendelezwa na mtafitiwa, Mz3, katika mfano wa hapo awali (uk. 55), wanapozungumza na rafikiye. Mtafitiwa huyu anasisitiza matumizi ya Kĩndia akiwa na nia ya kusisitiza utambulisho na kundi la kijamii la Wandia. Anaeleza kuwa anajivunia kuzungumza Kĩndia kwa kuwa hiyo ndiyo lugha ambayo amefunzwa kutoka utotoni; “*rĩrĩa ngwaria Kĩndia njĩgũaga njĩganĩire tondũ nĩyo lugha ndarutirwo kuuma ũnini wakwa*” (Wakati ninapozungumza Kĩndia huwa nahisi nikiwa mkamilifu kwa sababu ndiyo lugha niliyofunzwa kutoka utotoni) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 83).**

Hali hii ya watafitiwa kusisitiza matumizi ya lahaja zao, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ, ilijitokeza kwa wingi kwani watafitiwa walidai kwamba kutokana na kuishi pamoja na wazungumzaji wa Kikikuyu kwa muda mrefu kuna uelewano baina yao. Hivyo wao hawakuona haja ya kubadili usemi wao. Watafitiwa walitaka kudumisha matumizi ya lahaja zao ile zisije zikafifia. Badala ya kubadili usemi na kuchukua vipengee vya lugha ya Kikikuyu, watafitiwa waliamua kutumia lugha ya Kiswahili ili kufanikisha mawasiliano. Wazungumzaji wanapoendeleza utofauti au mwachano

baina yao na wanaozungumza nao ni ishara kuwa wanataka kusesitiza utambulisho wao kama kundi la kijamii. Hata ingawa lugha peke yake haiwezi kumtambulisha mzungumzaji, wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ walikuwa na mtazamo kuwa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ni muhimu katika utambulisho wao kama Wakĩrĩnyaga. Hivyo basi, watafitiwa wanaamini kuwa matamshi yao yanawapa utambulisho wao wa kijamii. Hata hivyo, kuna wale watafitiwa waliendeleza mfanano kwa kupunguza utofauti katika mazungumzo ili kufanikisha mawasiliano. Pia, kwa kubadili usemi wao kufanana na wanaozungumza nao wanajijengea silka za kutaka kukubalika na kutambulishwa na kundi la kijamii. Wanaoendeleza mfanano, wanataka kutathminiwa kama wanachama wa kundi la kijamii bila kubaguliwa na kudhalilishwa

4.3.2 Mitazamo ya Watafitiwa kuhusu Ubadilishaji Lugha

Katika sehemu hii, mtafiti alilenga kubaini mitazamo waliyokuwa nayo watafitiwa kuhusu ubadilishaji usemi hasa wanapotangamana na Wakikuyu katika mazungumzo. Katika kubaini mitazamo hii, mtafiti alijaribu kubaini pia sababu watafitiwa wanazoambatinisha na mitazamo yao kuhusu ubadilishaji wa usemi katika mazungumzo.

Jedwali 5: Asilimia ya watafitiwa walio na mitazamo chanya na hasi kuhusu kubadilisha lugha kama njia ya kuafikiana

| Watafitiwa | Jumla | Idadi ya waliokubali | % chanya | Idadi ya wasiokubali | % hasi |
|---------------------------|-------|----------------------|----------|----------------------|--------|
| Wazungumzaji wa Kĩndia | 24 | 10 | 41.7 | 14 | 58.3 |
| Wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ | 24 | 8 | 33.3 | 16 | 66.7 |

Kutokana na matokeo katika jedwali ni dhahiri kuwa asilimia 41.7 ya watafitiwa wa Kĩndia na 33.3 ya watafitiwa wa Kĩgĩchũgũ walikuwa na mtazamo chanya kuhusu ubadilishaji msimbo kwa sababu ya kusesitiza utambulisho. Kwa kubadilisha usemi wake, mzungumzaji anajaribu kuendeleza maafikiano au kukaribiana na mshiriki mwenzake kama jinsi ambayo inashinikizwa katika nadharia ya ukaribiano wa kimawasiliano. Ubadilishaji wa usemi unategemea washiriki

wanaohusika katika mazungumzo. Mazingira alimo mzungumzaji huchangia katika mabadiliko ya usemi kwani unapokuwa mazingira ambamo wazungumzaji wa Kikikuyu ni wengi kwa mfano huko Kiambu ama Murang'a mzungumzaji atajaribu kuzungumza kama wao kuashiria umoja. Kwa mfano, mtafitiwa mmoja alisema, “*ingĩthie mĩena ya Murang'a kĩwĩra rĩ nĩngeragia kwaria Gĩkuyu tondu nĩko kĩrario nĩ aikari acio*” (ninapoenda maeneo ya Murang'a kikazi huwa najaribu kuzungumza Kikikuyu kwa sababu hicho ndicho kinacchozungumzwa na wakaazi wa huko) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 84**). Pia katika kauli hii, “*riria ndaikaraga Kitale twaikaranagia na 'Aha' aingi na maingi ndaragia Kihhi nigetha tuelewane nao*” (nikiwa Kitale niliishi pamoja na Wakikuyu wengi hivyo wakati mwingi nilizungumza Kikikuyu ili tuelewane) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 84**). Watafitiwa hawa wana hisia kuwa kuna haja ya kubadili usemi ili kuleta maafikiano au ukaribiano hutokea katika mazingira mageni. Katika utafiti huu wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanadai kuwa wanapoenda katika mazingira mengine yalio na wazungumzaji wa Kikikuyu huwa wanazungumza Kikikuyu ili kuwe na maafikiano. Maafikiano haya yanaendelezwa ili kusisitiza na kukubalika kama wanajamii wa jamii la Wakikuyu.

Asilimia 58.3 ya watafitiwa wa Kĩndia na asilimia 66.7 ya watafitiwa wa Kĩgĩchũgũ walikuwa na mtazamo hasi kuhusu kubadili lugha ili kukubalika katika kikundi cha kijamii cha Wakikuyu. Kwa mfano, kulikuwa na matamshi kama, “*Turekira lugha citu iremba niki?*” (Kwa nini tunavisha lugha zetu vilemba) (**Rejelea Kiambatisho J, uk. 87**). Kauli hii ina maana kuwa mtafitiwa ana mtazamo hasi kuhusu kubadilisha lugha yake. Watafitiwa walisisitiza kuwa wao huendeleza utambulisho wao kama Wakikuyu kwa sababu ya utamaduni sawa na kuwa sio lazima wabadili msimbo ili kukubalika. Sababu kuu ya kuendeleza mitazamo hasi kuhusu ubadilishaji wa kusemi ni kwamba watafitiwa wanadai kuwa bali na kutumia lafudhi tofauti, kuna uelewano kati yao na wazungumzaji wengine wa Kikikuyu.

Mtafitiwa mmoja alisema kwamba yeye hawezi kubadilisha jinsi anavyozungumza kwa sababu hangependa kudhalilishwa. Madai haya ya kudhalilishwa kwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ilikuwa ni hali iliyobainika katika mahojiano ambapo watafitiwa wengine walisema kuwa wakati mwingi hudhihakiwa hasa wakiwa katika maeneo mengine ya mkoa wa kati. Hivyo basi hawaoni haja yao kubadili usemi kwa sababu wanadai kuwa wao ni wenyeji, kama

inavyobainika katika kauli hii;” *nĩkĩ gĩgūtũma ndũike nĩ nĩngũchenjia ũrĩa ndĩraria? O nĩo magĩrĩrwo gũchenjia tondũ nĩo ageni gũkũ na Andia nĩo aingĩ?* (Kwa nini mimi ndiye ninabadilishe jinsi ninavyozungumza? Kwa nini wao wasibadilishe ilhali wao ndiyo wageni katika maeneo yaliyo na wazungumzaji wa Kĩndia?) (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 84**). Watafitiwa hawa wanajivunia lahaja zao zinazozungumzwa katika maeneo yao, Kirinyaga, hivyo wanasisitiza lahaja hizi, Kĩndia na Kĩgĩchũgũ zizungumzwe.

Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wanazithamini lahaja zao na kuzionea fahari ndiposa hawaoni haja ya kubadili usemi wao kuzungumza Kikikuyu. Walisisitiza kwamba wakianza kuzungumza kama Wakikuyu wengine na kupuuzwa lahaja zao basi kuna hatari kwamba lahaja hizi za Kĩndia na Kĩgĩchũgũ zitafifia. Maoni haya yanaingiliana na yale ya Crystal (2000), anaposema kuwa watumizi wa lugha wanapoanza kupunguza matumizi ya lugha kimawasiliano, lugha hiyo hudhoofika na huanza kupoteza misamiati, wasemaji wake hupunguka na mwishowe huishia kufa. Hivyo ni muhimu kwa watafitiwa kuzungumza Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ili waweze kizidumisha na kuziendeleza kwa vizazi vya baadaye. Mtafitiwa mmoja alisema kuwa yeye kama mzungumzaji wa Kĩgĩchũgũ anajivunia lugha yake, hivyo hawezi kubadilisha na kuzungumza ‘*Kĩhaha*’ yaani, Kikikuyu, wakati wowote ule. Aliendelea kusema kuwa kama hakuna uelewano kabisa na anayezungumza naye, basi ni heri azungumze kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kwa mtazamo wake ni vigumu au nadra kwa Mũgĩchũgũ kubadilisha lugha yake akilinganishwa na Mũndia. Hata hivyo, ilibainika kuwa katika muktadha wa kimazungumzo, wazungumzaji wa Kikikuyu wakiwa wengi kuliko wale wa Kĩndia au Kĩgĩchũgũ basi inamlazimu mshiriki huyo kubadili usemi ili kufanana. Hivyo basi inabainika kuwa matumizi ya lugha hutawaliwa na wahusika wanaoshiriki katika mazungumzo na pia uhusiano wao. Hata ingawa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ walidai kuwa hawabadili lugha, ilidhihirika kuwa kati yao, kuna wakati wanabadili jinsi wanavyozungumza bila ufahamu wao. Kwa mfano mmoja wa watafitiwa alisema,

Dondoo 10: Tunukuzi kutoka mahojiano;

kwĩ bĩndĩ njĩraguo nĩndĩraria tofauti na mũno rĩra ngũarĩa na aciari makwa, arĩa maikaraga Gĩchũgũ. Gũkũ Mwea nĩnjikarĩte kwa ibinda rĩnene na andũ ma kabira ingĩ ta Andia na Akabete na nĩkĩo njĩragwo ndĩraria tofauti, no bakwa rĩ njũĩ kĩrĩa ndĩraria nĩ

Gĩcũgũ. (kuna wakati nimeambiwa kwamba ninazungumza kwa utofauti hasa ninapozungumza na wazazi wangu, ambao wanaishi Gichugu. Kwa kuwa nimeishi katika maeneo ya Mwea kwa muda mrefu na kutangamana na wazungumzaji kutoka makabila tofauti nchini na hasa Wandia na Akabete, inasababisha mimi kusikika kuzungumza tofauti ila kwa ufahamu wangu ninachozungumza ni Kĩgĩchũgũ) TY (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 84**).

Kutokana na kauli ya mtafitiwa huyu, kusikika kuzungumza kwa utofauti kunatokea bila hiari. Hata hivyo, kuna wanaodai kwamba wanabadili kwa hiari kwani wanajaribu kuiga kile ambacho kitafurahisha washiriki wenzao katika mazungumzo. Kwa mfano, mtafitiwa alisema,

Dondoo 11: Tunukuzi kutoka mahojiano;

rĩmwe nĩngwaria kĩhĩhĩ ta rĩu njuge (atĩrĩrĩ, ũka haha rĩu rĩ mũkuga atĩa!) no nĩ kwĩyarithia o aigue ndĩraria take akene, no tĩ bingo ciothe rĩmwe ngwaria ũguo nĩguo tũnyitanĩremuno angikorwo aria muraria nao aingi ni ma ‘hihi’ onakorwo ndikũhota kwaria take mũũno. (Wakati mwingine nitazungumza ‘*Kĩhĩhĩ*’ kimaksudi nisikike kuzungumza kama yeye na arithike, hata hivyo wakati mwingine nitazungumza hasa kama kuna wazungumzaji wengi wa Kikikuyu ndiposa kuwe na uelewano hata ingawa sitaweza kuzungumza kama yeye kwa usemi halisi). (**Rejelea Kiambatisho I, uk. 83**).

Kutokana na kauli ya mtafitiwa huyu ni dhahiri kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ huzungumza kwa kuiga Kikikuyu kwa sababu wanataka kuendeleza maafikiano katika mazungumzo. Wanaafikiana kwa kujaribu kupunguza tofauti zilizopo kati ya kilahaja.

Wengine wa watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa ili mzungumzaji abadili lugha au jinsi wanavyozungumza lazima awe ameishi katika maeneo ya wazungumzaji wa lugha au lahaja husika kwa muda mrefu. Inadhihirika kuwa watafitiwa wana hisia kuwa ukaribiano wa kiisimu utatokea bila ufahamu na pia mzungumzaji atabadili ruwaza zake za mazungumzo akiwa katika mazingira haya ili kukubalika na kurahisisha uelewa katika mazungumzo. Watafitiwa hawa wanaamini kuwa mabadiliko ya kiisimu hutokea kwa sababu ya athari za mazingira geni kwa sababu kuna haja ya kukubalika katika mazingira hayo na kuendeleza mawasiliano mwafaka.

Asilimia 37.5 ya watafitiwa walikuwa na mtazamo kwamba kuna haja ya kubadili jinsi mtu anavyozungumza ili kukubalika. Walio na mtazamo huu wanakubali kuwa mabadiliko ya kiusemi yanapaswa kutokea kama mzungumzaji anayehusika ameishi katika maeneo k.v ya Nyeri, Murang'a na Kiambu. Watafitiwa wanaamini kuwa mzungumzaji anatarajiwa kuzungumza lugha inayotumika katika maeneo anamoishi ili kuonyesha umoja na ushirikiano. Pia ilibainika kuwa ubadilishaji usemi unategemea washiriki walio katika mazungumzo. Kama wanaozungumza Kikikuyu ni wengi kuliko wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ basi kuna haja kubadili ili kuafikiana kama inavyodhihirika katika kauli ifuatayo; “*Angĩkorwo arĩa mūraria nao aingĩ nĩ Akabete no mũhaka ũrĩaria tao nĩguo wĩtĩkĩrĩke ta ũmwe wao.*” (kama mnaozungumza nao wengi ni Wakikuyu basi ni lazima mtu kubadili jinsi unavyozungumza ili ukubalike kama mmoja wao) **(Rejelea Kiambatisho I, uk. 83).**

Inapofikia hatua kwa wazungumzaji wa lugha au lahaja fulani kukubali kuacha kutumia lugha yao na kuanza kuzungumza lugha au lahaja ya wanajamii wengine, basi mfanano wa kiisimu huendelezwa kama wanavyosisitiza Giles na Coupland (1991). Ilibainika kuwa lengo kuu la kutaka kubadili jinsi mzungumzaji anavyozungumza ni maafikiano na kumfurahisha mshiriki mwenzake katika mazungumzo. Mzungumzaji analenga kukuza mazingira ambayo yatadumisha mahusiano baina yake na wanaoshiriki katika mazungumzo. Hali hii hudumisha mshikamano wa kijamii kati ya wanaohusika katika mazungumzo. Kati ya wale wanaokubali kubadilisha lugha au usemi, kuna walio na madai kwamba wanaepuka kuzungumza lahaja yao wakiwa miongoni ya Wakikuyu wengine ili kuficha aibu au kudhihakiwa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, dhana tafitiwa ambazo zimedhihirika katika sura zilizotangulia zinaangaziwa. Sura hii imegawika katika sehemu tatu; kwanza ni muhtasari wa matokeo ya utafiti unaorejelea madhumuni ya utafiti, hitimisho la utafiti na mwisho inaweka bayana mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

5.2 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mitazamo ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kuhusu utambulisho wao na michakato ya kiukaribiano wanayoendeleza kuafikiana na kuunda utambulisho wao wa kijamii. Utambulisho wa kijamii unahusisha wale watu katika jamii wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wanatokana na jamiilugha ambayo iko tofauti na jamiilugha nyingine (Tajfel & Turner, 1979).

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ wana mitazamo chanya na hasi kuhusu utambulisho wao na wanajamii wa jamii ya Wakikuyu. Watafitiwa walikuwa na mitazamo kuwa kipengele muhimu katika utambulisho wao wa kijamii hauzingatii lugha tu bali pia historia, desturi, mila na utamaduni wao ambao unafuatwa na kila mwanajamii. Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kudhaniwa kuwa wao si Wakikuyu kunatokana na namna wanavyozungumza. Hata hivyo walikuwa na mtazamo kuwa kuna uelewano kati yao, hivyo hawafai kutengwa kama Wakikuyu kwa sababu ya lafudhi wanayotumia. Hata hivyo, asilimia 27 ya watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa wao ni Wakĩrĩnyaga wala sio Wakikuyu. Kwa watafitiwa hawa kutaka kujitambulisha kama Wakĩrĩnyaga ni kwa sababu wanahisi kwamba wanatengwa na hajawahi kubalika na Wakikuyu wenzao kama watu wa kundi moja. Ndiposa kulikuwa na kauli kama vile, *“ithuĩ tũhuana ta maĩ me irũtũinĩ.”* (Ikiwa na maana kwamba wananing’inia tu kama yale maji yanayokuwa katika jani la mmea wa *nduma*), yaani hawakubaliki kama wamoja na Wakikuyu wala Waembu. Ndiposa kuna walio na mtazamo kuwa

kuna haja wao wapewe hadhi ya kuwa kundi tofauti sababu wana lugha na utamaduni ulio tofauti na ule wa Wakikuyu. Pia wanahisi kuwa lugha na utamaduni wao uko katika hatari ya kufifia hivyo wangetaka kutambulishwa kama kundi la kijamii mahsusi ili kuweza kuhifadhi utamaduni wao kwa vizazi vya kesho. Matokeo haya yanaungwa mkono katika nadharia ya ukaribiano wa mawasiliano ya Giles (1982), inayoeleza kuwa utambulisho wa jamii huweza kutoweka ikiwa watumiaji wake wataacha kutumia lugha yao na kutumia lugha nyingine.

Asilimia 70 ya watafitiwa walikubali na kusisitiza kwamba wangependa kutambulishwa na jamii ya Wakikuyu wala sio Waambu au Wameru. Wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ walijiona na kujitambua kuwa tofauti na jamiilugha za Waambu na Wameru katika maswala ya lugha, utamaduni, mila na desturi.

Mitazamo hasi ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ ilitokana na madai kuwa wanatengwa na kudhalilishwa na Wakikuyu wenzao katika maswala mbalimbali. Lugha ni chombo cha kuwaunganisha au kuwatenganisha au kuwabagua watu (Edwards, 2009). Kauli hii inawiana na matokeo ya utafiti kwani ilibainika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ hutengwa na kubaguliwa na Wakikuyu wenzao kutokana na lafudhi wanayotumia. Haya yanashahibiana na maoni ya Lambert (1967), anaposema kuwa watu hutathmini wengine kwa njia ya uchanya au uhasi kutokana na namna wanayozungumza na kuendeleza mitazamo mbalimbali.

Watafitiwa katika utafiti walijitambulisha kwanza na lahaja wanayozungumza kwa mfano, “*nĩ ndĩ Mũndia*”, “*nĩ ndĩ Mugĩchũgũ*” (mimi ni Mundia, mimi ni Mugĩchũgũ). Hata hivyo, wengi wao walikuwa na ufahamu kuwa “*Mũndia*” na “*Mũgichũgũ*” ni mwanajamii ya Wakikuyu. Kuhusu utambulishaji na jamii lugha ya Wakikuyu, ilibainika kuwa watafitiwa walikuwa wakijinasibisha na jamii hii, ya Wakikuyu, kutokana na mifumo sawa ya kitamaduni ikiwemo masuala ya ndoa, utaratibu wa kuwapa watoto majina na mifumo ya kiukoo. Kwa kujinasibisha na koo kama vile ya *mumbui*, *mugaciku*, *munjiru* na nyinginezo

Kutokana na matokeo ya utafiti ilidhihirika kwamba mitazamo hasi na chanya kuhusu ubadilishaji wa usemi huathiri uteuzi wa matumizi ya lugha katika mazungumzo na watafitiwa. Baadhi ya watafitiwa waliokuwa na mitazamo chanya walikuwa wakibadili usemi wao kwa sababu ya kuendeleza mshikamano na umoja kati yao na wanajamii lugha husika. Ilibainika kuwa

matumizi ya lugha yaliathiriwa na idadi ya wazungumzaji waliohusika katika mazungumzo. Kwa mfano kama idadi ya washiriki wanaozungumza Kikikuyu walikuwa wengi basi ilimlazimu mzungumzaji wa Kĩndia au Kĩgĩchũgũ kubadili usemi ili kufanikisha mawasiliano na kukubalika kama mmoja wao. Pia mazingira alimo mzungumzaji yalikuwa kigezo cha mzungumzaji kubadili usemi. Idadi kubwa ya watafitiwa walikuwa wanatumia lahaja yao, iwe ni Kĩndia au Kĩgĩchũgũ, kuwasiliana na wanajamii wenzao hivyo kuisisitiza utambulisho wao kama Wakĩrĩnyaga. Hata hivyo, kulikuwa na kuchanganya usemi wakati wazazi walikuwa wakizungumza na watoto wao. Walidai kwamba wakati mwingi huzungumza na watoto kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa hiyo ndiyo lugha ambayo wanatumia wakiwa shuleni. Hali hii iliwahuzunisha wazee wengi waliohojiwa kwa kuwa walidai kuna hatari kubwa kwa lugha na jamii ya Wakikuyu kwa kuwa wanafisha lugha na utambulisho wao kama Wakikuyu. Hivyo walisisitiza kuwekwe mikakati ambayo itasaidia kudumisha lugha ya Kikikuyu kama vile masomo ya TKK katika mashule na pia wazazi kuwa katika mstari wa kwanza kufunza watoto wao lugha yao.

Kwa upande wa matumizi ya lugha, utafiti ulibainisha kwamba watafitiwa wanaendeleza ukaribiano wa kiisimu wakati wa mtagusano wa kilahaja ili kuafikiana. Watafitiwa walidai kuwa kuzungumza Kikikuyu hutokea bila hiari kwa wakati mwingi ila kuna wakati ni kwa hiari. Wanaodai kwamba hali hii hutokea kwa hiari wanasema kwamba huwa hawatambui wamebadili bali wanaelezwa na wasikilizaji au wanaozungumza nao. Kwa upande mwingine, wengine wanazungumza Kikikuyu wakiwa na nia tu ya kufurahisha mzungumzaji anayehusika kuwa anaweza kuzungumza kama yeye na wakati mwingine anataka atambuliwe kama Mkikuyu. Katika mchakato wa mfanano, mabadiliko katika sauti /h/ ndiyo yaliendelezwa kwa kiwango kikubwa. Kwa kujaribu kufanana na wazungumzaji wa Kikikuyu, watafitiwa walibadili matumizi yao ya /b/ na badala yake kutumia sauti /h/. Hata hivyo asilimia kubwa ya watafitiwa walikuwa na mtazamo kuwa hakuna haja ya kubadili usemi wao isipokuwa wakati hakuna uelewano katika mazungumzo. Hivyo basi, mwachano au utofauti ndiyo mchakato ulioendelezwa na asilimia kubwa ya watafitiwa.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulikuwa ni hatua ndogo katika kuelewa matumizi ya lugha na utambulisho wa kijamii. Katika utafiti huu ilibainika kuwa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ husisitiza na kudumisha utambulisho wao kama Wakikuyu. Kwa kujiainisha na jamii ya Wakikuyu wanatambua kuwa kuna vibainishi vinavyowafungamanisha na jamiilugha ya Wakikuyu vikiwemo lugha, utamaduni, mila, desturi na historia. Lugha na utamaduni ni vipengele ambavyo vilidhihirika kuwa ni amali muhimu katika utambulisho wa kijamii wa wazungumzaji Kĩndia na Kĩgĩchũgũ. Hivyo, wazungumzaji walijitambulisha kwa koo mbalimbali ili kusesitiza utambulisho wao na jamii ya Wakikuyu. Koo hizi ni kama zifuatazo; *Anjiru, Ambũi, Agacikũ, Aceera, Angarĩ, Ethaga, Aithĩrandũ, Airimũ, Angũi na Aicakamũyũ*.

Hata hivyo, wakati mwingine mzungumzaji hutengwa na kudhalilishwa kutokana na lafudhi anayotumia jambo ambalo husababisha mitazamo mbalimbali. Hata ingawa wanatengwa na kudhalilishwa watafitiwa walisisitiza kuwa wao ni wanajamii wa jamii ya Wakikuyu kwa sababu ya utamaduni mmoja hasa dhana ya kuendeleza koo zile tisa kamilifu zinazowapa utambulisho wao wa kijamii kama Wakikuyu. Udhalilishaji huu huwa sababu mojawapo ya wao kukanwa kuwa si Wakikuyu. Kwa kuwa wanakanwa kuna watafitiwa walioendeleza mtazamo kuwa ni muhimu wajitenge kama jamii lugha tofauti na ile ya Wakikuyu na kutambuliwa kama Wakirinyaga.

Katika mazungumzo, mtu huchagua lugha ambayo italenga mahitaji yake na hutegemea uhusiano uliopo kati ya wanaoshiriki katika mazungumzo. Kwa kuwa lahaja za Kĩndia au Kĩgĩchũgũ huwa hazitumiki katika elimu, siasa na vyombo vya mawasiliano, asilimia tisini ya watafitiwa wazee walisisitiza matumizi ya Kĩndia au Kĩgĩchũgũ kimawasiliano kwa lengo la kuzidumisha ili zisije zikafifia. Hata ingawa wanasisitiza kutumia lahaja hizi wanajiainisha na kujitambua na jamii ya Wakikuyu kutokana na kuwa na lugha, historia, utamaduni, mila na desturi sawa. Hivyo basi, kilicho muhimu katika utambulisho na jamii ya Wakikuyu ni uendelezaji wa utamaduni, mila, desturi, hisia na mitazamo sawa. Lugha ni zao la kijamii na kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii husika kwa kuwa inahifadhi amali za kijamii na kumwezesha mwanajamii kuwasiliana na kuendeleza utamaduni wake (Kingei, 2010; Schiffman 1996). Lugha hutumika

katika kurithisha mila na desturi za jamii. Binadamu huweza kufunzwa na kupewa maadili mbali mbali kwa kutumia lugha ili waweze kujitambua kuwa wao ni akina nani.

5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti

Utafiti huu ulikuwa ni hatua ya kutaka kuelewa mitazamo kuhusu utambulisho wa kijamii wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ kupitia matumizi ya lugha. Mitazamo yao ilikuwa muhimu katika kuelewa jinsi wanavyojitambulisha na kutumia lugha. Kwa hili mtafiti anapendekeza yafuatayo:

- a) Kwanza, utafiti zaidi ufanywe kuhusu lugha na utambulisho wa kijamii baina ya wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ na jamii lugha zingine zinazopatikana katika maeneo ya Mwea. Utafiti kama huu utaendeleza maarifa katika isimujamii kuhusu mtagusano wa lugha na jinsi wanavyoendeleza dhana ya utambulisho.
- b) Pili, utafiti utakaolenga kuchunguza matumizi ya lugha na utambulisho kati ya wazungumzaji wa Kĩgĩchũgũ na Kĩndia wanaopakana na Waembu na Wakamba mtawalia.
- c) Tatu, utafiti zaidi utakaochunguza matumizi ya lugha na utambulisho wa kijamii unaohusisha wazungumzaji wa lahaja za lugha mbalimbali za jamii lugha zingine katika nchi ya Kenya.
- d) Nne, utafiti utakaolenga kuchunguza lugha na utamaduni katika kubainisha utambulisho wa kitamaduni wa wazungumzaji wa Kĩndia na Kĩgĩchũgũ.

MAREJELEO

- Bhat, M. (2017). *The changing roles and linguistic identities of the Kashmiri speech community*. Cambridge Scholars Publishing.
- Blacker, J. (2007). The demography of Mau Mau: Fertility and mortality in Kenya in the 1950s: A demographer's viewpoint. *African Affairs*, 106(423), 205-227.
<https://www.jstor.org/stable/4496439>
